# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 09 | Oktoba 30, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO




# MIZIZI YA RISHI KENYA

**Waziri Mkuu mchanga zaidi Uingereza katika zaidi ya karne mbili ameiweka Kenya, nchi alikozaliwa baba yake, katika ramani ya dunia, alivyofanya Obama. Je, nafasi yake itaboresha uhusiano kati ya Kenya na Uingereza?**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

## anywhere, anytime.




Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

# Yaliyomo

**8 NDOTO AU UKWELI?** Hatua inayofuata baada ya mafuta kupatikana Kaskazini ya Kenya inahusu uchimbaji ambao ni ghali na mradi wa bomba. Je, Tullow PLC itaendelea na mradi huu, kushirikiana na kampuni nyingine au itauzia shirika lingine?

**10 LESENI YA KUUA:** Kikosi cha Huduma Maalumu kilichovunjwa cha Idara ya Upepelezi wa Jinai ni kimoja tu cha vikosi vingi ambavyo vimetesa Wakenya kwa miaka mingi. Maafisa hao hawachukuliwi hatua na wao ndio sheria.

**18 MUZIKI KWA MAMILIONI:** Kupanuliwa kwa majukwaa ya utiririshaji katika Afrika kunamaanisha pesa zaidi kwa wanamuziki wa Kenya



**22 MAJUKUMU YAKIWA KINYUME:** Mume wa Gavana akijihusisha na shughuli za mke wake, analaumiwa kwa kuingilia mambo yasiyomhusu. Kanuni hiyo haitumiwi kwa Wake wa Magavana, ambao wanahusika sana katika shughuli za waume wao.

# Lazima tuwasaidie kina Obama na Rishi kati yetu kufaulu katika siasa

Video katika YouTube yenye kichwa 'Jinsi nchi hii ya Afrika inavyotawala Ulimwengu' imezua msisimko katika mitandao ya kijamii. Ilitolewa baada ya Rishi Sunak kuteuliwa kiongozi wa chama cha Conservative na Waziri Mkuu wa Uingereza, na inaorodhesha watu kadhaa maarufu ulimwenguni ambao wana mizizi Kenya.

Baba ya Bw Sunak anatoka Kitale, baba ya aliyekuwa Rais wa Amerika, Barack Obama anatoka K'Ogelo, kisha kuna nyota wa Hollywood, Lupita Nyong'o, binti ya Gavana wa Kisumu, Anyang'Nyong'o.

Katika orodha hiyo pia kuna Malaika Firth, mwanamitindo mashuhuri, Eddy Gathegi,

Muigizaji wa Hollywood, Wangari Maathai, mshindi wa tuzo ya Amani ya Nobel, Roger Whittaker, mwanamuziki, Victor Wanyama, mwanasoka, Richard Leakey, mwanapaleontolojia na Eliud Kipchoge, bingwa wa mbio za marathon.

Swali ni: Kama Kenya inaweza kutoa watu hawa wote maarufu ambao wanatawala vyema nchi zenye nguvu, taaluma na biashara ulimwenguni, kwa nini humu nchini uongozi ni hafifu, na pengine mbaya zaidi? Ni bayana kuwa sio kosa la jeni; jeni za Wakenya zinaonekana kuwa miongoni mwa bora zaidi. Je, kuna uwezekano tulipeleka nje zile bora na kuacha makapi nyumbani kuendesha masuala ya chanzo hiki cha binadamu?

### Uzembe hauvumiliwi

Inawezekana kuwa mazingira katika nchi hii yanakuza udhaifu na ufisadi. Mkenya anayeendesha gari Nairobi atapita kando, kupiga honi, kuwa mtundu au jeuri barabarani.



Mutuma Mathiu

**Kama Kenya inaweza kutoa watu hawa wote maarufu ambao wanatawala vyema nchi zenye nguvu, taaluma na biashara ulimwenguni, kwa nini humu nchini uongozi ni hafifu, na pengine mbaya zaidi? Ni bayana kuwa sio kosa la jeni; jeni za Wakenya zinaonekana kuwa miongoni mwa bora zaidi. Je, kuna uwezekano tulipeleka nje zile bora na kuacha makapi nyumbani kuendesha masuala ya chanzo hiki cha binadamu?**

Mkenya huyo akiendesha gari Ujerumani atakuwa mfano wa kuigwa kwa heshima barabarani, mtiifu wa sheria za trafiki, mvumilivu na kudumisha usalama wake na madereva wengine.

Mkenya huyo anaporudi nyumbani, atabadilika kuwa shetani tena, akinyanyasa wanaotembea kwa miguu na kuweka maisha ya watu hatarini. Tofauti ni kuwa, katika nchi hizo zingine, ufisadi, uwezekano wa hongo na uzembe hazivumiliwi; bidii, maadili mema na ushindani zinakuzwa.

Kutokana na miktudha hiyo, Wakenya na uzao wao wanazingatia na kufaulu. Ni desturi, matarajio na viwango vinavyoamua matokeo bora.

Kinyume ni hayo, matarajio nyumbani yako chini sana, kama yapo. Sura ya Sita ya Katiba inajaribu kuweka viwango vya uongozi bora, lakini hivyo vinapuuzwa kila wakati hali inavyobadilika. Panapopatikana viwango, viko chini sana kuleta tofauti yoyote.

Hivyo basi, watu wanaoshukiwa kwa makosa mabaya, walio na historia ya uhalifu au wanaokabiliwa na mashtaka mabaya katika korti za kisheria, wanateuliwa kushikilia ofisi kubwa na kupitishwa na Bunge la Kitaifa.

### Maadili chanya, yenye nguvu

Kuna dhana ya kutokuwa na hatia, bila shaka. Kila mshukiwa hana hatia hadi ithibitishwe katika korti ya kisheria. Lakini wakati huo huo, ni busara kudhania kuwa pale mtu ameshtakiwa katika korti ya kisheria, mtu kama huyo anabaki asiyefaa kuteuliwa kushikilia ofisi kubwa hadi atakapoondolewa lawama na korti, kisha anaweza kuendelea na maisha ya kawaida.

Kenya inahitaji kuchukulia masuala ya maadili kwa makini zaidi ili siasa ziache kuwa mwanzo na mwisho.

Maadili chanya muhimu kama vile uaminifu, uzalendo na kufanya kazi kwa bidii yanafaa kukubaliwa na kutarajiwa kuwa vipimo vya uongozi kuliko uwezo wa kulimbikiza utajiri kwa njia haramu na kutumia pesa kiholela. Wakenya wako na jeni nzuri lakini wana maadili mabaya. Hii ndiyo sababu hii bado ni nchi inayoendelea.

***mmutuma@ke.nationmeia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Mutuma Mathiu** Mhariri Mkuu
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Wabunge kupiga msasa makatibu wateule

# Mawaziri wapya tayari kuanza kazi

Huku mawaziri 22 wa Rais William Ruto hatimaye wakiapishwa kuingia ofisini baada ya kupigwa msasa na kuidhinishwa na Bunge la Kitaifa, mawaziri hao wiki hii wanatarajiwa kuanza kazi katika wizara zao husika.

Walitumia Alhamisi na Ijumaa wiki jana kuchukua ofisi zao kutoka kwa watangulizi wao baada ya kuapishwa kuanza kazi.

Pia, macho yote yatakuwa kwa kiongozi wa nchi atakapowasilisha bungeni majina ya makatibu wateule ambao watasimamia Idara tofauti za serikali.


Rais anatarajia kupokea majina hayo kutoka kwa Tume ya Utumishi wa Umma, ambayo imekuwa ikiwahoji watu zaidi ya 500 walioorodheshwa baada ya kutuma maombi na hatimaye ikateua 49 pekee.

Majina hayo yatakabidhiwa kamati za Bunge la Kitaifa. Kabla ya hapo, Kamati za Bunge zitakutana kuchagua viongozi wake, ambao ni wenyekiti na manaibu wenyekiti ili ziweze kuanza shughuli ya kuwapiga msasa.




Waziri wa Mazingira na Misitu Soipan Tuya akiapishwa katika Ikulu ya Nairobi, mnamo Oktoba 27. PICHA | DENNIS ONSONGO

■ Bingwa McIlroy ahofia utengano "usiorekebika"



Phil Mickelson wakati wa Pro-Am kabla ya mashindano ya LIV Golf, uwanja wa gofu wa The Oaks, Massachusetts, Septemba 1. PICHA | AFP

# Mickelson asema LIV haitasambaratika

Mshindi mara sita Phil Mickelson anasema shindano lililojitenga linaloungwa na Saudi Arabia la LIV Golf Series ni "kubwa katika mchezo huo ambalo haliendi popote" baada ya bingwa wa dunia Rory McIlroy kueleza hofu ya mgawanyiko usioweza "kurekebishwa". Msimu wa LIV unafikia tamati katika Trump National club, Doral, karibu na Miami, wikendi hii kwa shindano la makundi kuwania zawadi ya dola 50 milioni.

Uhasama ambao kujitenga kwa LIV umesababisha umeacha McIlroy na wasiwasi kuhusu mchezo huo. Katika hafla ya wanahabari ya kuzindua, Mickelson alisema LIV Golf tayari imekaidi matarajio na itaendelea. "Ninatazama LIV Golf na tulipo wakati huu, tulipokuwa miezi sita, saba iliyopita, watu waliposema hii imekufa, na tumepita hayo, na tuko hapa leo, nguvu katika mchezo huu na hatuondoki," akasema.

Akiketi jukwaani na mshindi wa British Open, Cameron Smith, mshindi wa zamani wa Masters, Bubba Watson na Ian Poulter, aliyepigiwa debe katika English Ryder Cup, Mickelson alisema ubora wa talanta katika LIV "unapeleka taaluma ya gofu kote ulimwenguni. Ni hatua kubwa ambayo LIV Golf imepiga katika miezi sita, saba iliyopita. Sidhani kuna mtu yeyote anayeweza kupinga hilo," akasema Mwamerika huyo.

■ Ukaguzi ulifanywa 'miaka miwili iliyopita'

# Meghan ni 'asilimia 43 Nigeria'



Mke wa mwanamfalme wa Sussex amesema uchunguzi ulifichua "asilimia 43 ya mizizi yake ni Nigeria".

Kwenye tukio la hivi punde katika podcast yake, Meghan aliambia mtangazaji wa kipindi cha Nigerian-American, Ziwe Fumudoh, kuwa "uchunguzi wa nasaba yangu ulifanywa miaka miwili iliyopita". Fumudoh alipomuuliza "wewe ni nini?", Meghan alijibu kuwa "asilimia 43 ya asili yake ni Nigeria". "Nitachunguza zaidi kwa sababu kila ninayemwambia, hasa wanawake wa Nigeria hushangaa "Eti nini!" akaongeza.

■ Putin ajaribu kuhalalisha uvamizi wa Ukraine

# Dunia yapitia 'muongo hatari zaidi'



Dunia inakabiliwa na "pengine muongo hatari zaidi" tangu mwisho wa Vita vya Pili vya Dunia, Rais wa Urusi Vladimir Putin ameonya. Katika hotuba kwa nchi, Putin alijaribu kuhalalisha uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine, hatua ambayo imeacha nchi hiyo imetengwa na mataifa mengine duniani.

Putin pia alilaumu nchi za Magharibi kwa vitisho vya nuklia dhidi ya Urusi ili kulazimisha washirika wao kuitenga Urusi. Mataifa ya Ulaya yamekanusha madai hayo.

Mapema wiki hii, muungano wa kijeshi wa Nato ulilaani madai yasiyofafanuliwa ya Urusi kuwa huenda Ukraine ikatumia "bomu chafu"-vilipuzi vyenye kemikali hatari.

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ ISHARA YA MAFANIKIO KWA 'WALIOKATALIWA' AFRIKA MASHARIKI

# RISHI: KENYA HADI UINGEREZA

*Wazazi wa Waziri Mkuu walikuwa sehemu ya Wahindi "wasiokuwa na nchi" waliochukuliwa kuwa watu "wasiotakiwa" katika Himaya ya Uingereza na wakajitahidi hadi wakafika Uingereza - ambako mfumo uliobagua wahamiaji Waingereza wa asili ya Asia ulitumiwa*



Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak akizungumza wakati wa mara yake ya kwanza kushiriki kikao cha Bunge cha Mwaswali kwa Waziri Mkuu jijini London, mnamo Oktoba 26.

• Na JOHN KAMAU

Wazazi wa Waziri Mkuu wa Uingereza Rishi Sunak walipoondoka Kenya miaka ya 1960 -- haikuwa kwa kupenda kwao. Ahadi iliyotolewa na Kanu muda mfupi kabla ya uhuru, kuwa kungekuwa na "nafasi kwa kila mtu" ilikuwa kwa waliochukua uraia wa Kenya.

Nchini Kenya, Waingereza wenye asili ya Asia walichukuliwa kuwa tabaka la kati, lakini walipofika Uingereza waliruhusiwa tu kufanya kazi duni na walitajwa kuwa "watu wa rangi". Hatua hiyo ilinuiwa kuzuia waliotaka kuhamia huko.

Wazazi wa Waziri Mkuu walikuwa sehemu ya Wahindi "wasiokuwa na nchi" waliochukuliwa kuwa watu "wasiotakiwa" katika Himaya ya Uingereza na wakajitahidi hadi wakafika Uingereza - ambako mfumo uliobagua wahamiaji Waingereza wa asili ya Asia ulitumiwa

Uingereza iliruhusu idadi ndogo ya wahamiaji kwa mwaka, na ilikuwa imekubaliana na Jomo Kenyatta kuhusu idadi ya walioruhusiwa kuondoka Kenya, ambayo ilikataa kuwapa uraia wa nchi mbili.

Wakati wa makongamano ya Lancaster kuhusu Katiba ya Kenya, Kanu ilipinga pendekezo la Kadu la kuwapa watu uraia wa nchi mbili. Baada ya uhuru, wasiokuwa Waafrika Kenya walipewa miaka miwili kuamua. Raia wenye asili ya Asia walijipata kwenye njiapanda. Hawangerudi India - ambayo ilikuwa imewafungia milango - au kuchukua uraia wa Uingereza kwa urahisi kutokana na sera ya ubaguzi dhidi ya raia wa kigeni.

Akiwa daktari, baba ya Sunak, Yashivir, ambaye alizaliwa Kenya, na mama yake, Usha Sunak, mzaliwa wa Tanzania, aliyekuwa mfamasia, walikuwa wataalamu wa sekta ambayo ilinuiwa kutengewa Wakenya asili.

Ingawa Kenya ilikuwa na madaktari 38 Waafrika ilipopata uhuru, wanane wakijifunza kazi, hatima ya madaktari wa kigeni ilijadiliwa bungeni mnamo 1963, ambapo wabunge walishinikiza serikali kutengea Wakenya sekta ya afya. Wakati huo, Wizara ya Afya ilikuwa imeajiri madaktari 218 wa kimatibabu.

Ili kutamausha Wahindi wasiokuwa raia wa Kenya, serikali ya Kenyatta iliwakabili na sheria mpya zilizowalazimisha kuomba vibali vya kufanya kazi - kana kwamba walikuwa wahamiaji wapya - na watengewa kazi walizopaswa kufanya.

Ingawa serikali ilitaka kampuni kuwa na wakurugenzi wa humu nchini ili kuepuka kuandamwa, nyingi za biashara zilizomiliki-

...Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

# Familia ya Rishi ilivyofika Uingereza



**Rais wa kwanza wa Kenya, Jomo Kenyatta, akitia saini katika kitabu cha wageni katika majengo ya Bunge mnamo Februari 1975. Serikali yake iliwapa ilani makataa wafanyabiashara na walowezi Kenya: Wachukue uraia wa Kenya au wafanye mipango ya kuondoka na familia zao.**

Kutoka Uk 5

wa na Wahindi zilikuwa za kifamilia na hazingeweza kuajiri watu wengine. Kinaya ni kuwa, Wahindi waliofukuzwa kutoka biashara za reja reja walifungua viwanda, na ndiyo sababu yao kuwa wengi katika sekta hiyo.

Mwanzoni, kuanzishwa kwa tabaka la wafanyabiashara Waafrika kuchukua nafasi ya Wahindi waliokuwa wameitawala kulikumbwa na matatizo - na kuliumiza wengi waliokuwa wauzaji duka wa kawaida na wakalazimika kujiondoa sekta ya biashara reja reja.

Mkondo huu wa kisiasa ulikuwa umewekwa mnamo Mei 1960 na Tom Mboya, aliyeambia Bunge kuwa watu wanaotafuta "uaminifu maradufu lazima wawe na woga kwa sababu si Wakenya katika mioyo yao. Wanataka kutumia vibaya fursa hiyo... Iwapo anataka kuwa Mwafrika, na kuna nafasi ya Wahindi na Wazungu kuwa Waafrika, basi awe Mwafrika bila kuhitimu".

Baada ya uhuru, serikali ya Jomo Kenyatta iliwapa wafanyabiashara na walowezi wote Kenya makataa: Wachukue uraia wa Kenya au wafanye mipango ya kuondoka na familia zao. Kenya ilikuwa imeiga India, ambayo mnamo 1955 ilipitisha Sheria ya Uraia, ambayo ilikomesha uraia wa nchi mbili.

Mtu alipaswa kuamua kuwa raia wa India au raia wa Uingereza. Kisha iliweka sera ya kutokubali raia wa Asia waliokuwa na paspoti za Uingereza, na ni baadaye Julai 2017 ambapo walitambuliwa kuwa kabila jipya la Kenya – baada ya miaka 54 ya ubaguzi.

Kwa Kenyatta, ili kutekeleza sera hiyo mpya, serikali yake ililazimika kuanzisha Afisi ya Kupendelea Wakenya - ambayo jukumu lake lilikuwa kusimamia kuondolewa kwa wafanyakazi raia wa Uingereza na Asia katika sekta ya umma na ya kibinafsi na kupendekeza wapewe upya vibali vya kufanya kazi.

Walowezi wafanyabiashara na wakulima pia walipewa "ilani za kuondoka" ili kutoa nafasi za biashara kwa Waafrika na kuchukua mashamba ya walowezi, kuwa na Akiba ya Ardhi chini ya mpango wa utoaji makao.

Huku vibali vya kazi na Akiba ya Ardhi zikitumiwa kuendeleza ufisadi katika miaka ya 1960 na 1970, sera ya uhamiaji ilifurusha maelfu ya familia kutoka Kenya - na ikaunda kizazi kipya cha jamii zilizozaliwa Kenya na zikaenda kuishi ng'ambo.

Nyingi za familia hizo zilikuwa za wawekezaji na wafanyabiashara stadi, na leo baadhi yake zinamiliki viwanda Uingereza na Canada zilikohamia.

Hata hivyo, hatua hiyo ilizua hofu kubwa Uingereza - na kulazimisha Serikali ya Chama cha Labour kupitisha Mswada wa Wahamiaji wa Jumuiya ya Madola ili kupunguza idadi ya wahamiaji nchini humo.

Lengo lilikuwa kuzuia Wahindi kutoka Afrika Mashariki na watu wengine waliokuwa na paspoti za Uingereza wakiishi nchi za kigeni kuingia nchini humo.

Waziri wa Mashauri ya Ndani, James Callaghan, aliambia Bunge kuwa hatua hizo zilifaa "kwa kulinda haki za watu wa nchi hii na kwa maslahi ya usawa kwa raia wa Jumuiya ya Madola kwa jumula".

Alipendekeza kutengwa kwa vibali 1,500 vya ajira kila mwaka kwa waliokuwa na paspoti za Uingereza ambao walikuwa na uhusiano mkubwa na Uingereza ama kwa kuzaliwa au baba zao kuwa raia wa Uingereza.

Shida sasa ilikuwa Wahindi 35,000 nchini Kenya waliokuwa na paspoti za Uingereza na raia wengine 105,000 wa Asia ambao wangekosa kuwa wa taifa lolote.

Huku Kenyatta akiendelea na mpango wake wa kukumbatia Waafrika, Uingereza ilikuwa na hofu kuwa angewafukuza badala ya kufuata mfumo wa kuruhusu wachache kuishi Kenya.

Kupitia mpango wa kukumbatia Waafrika, familia nyingi za Kihindi zilipoteza mali na biashara kwa wanasiasa waliokuwa na ushawishi. Wengine, ambao hawakuwa wameacha uraia wa Uingereza baada ya uhuru, walilazimishwa kuondoka kupitia sheria zilizofanya vigumu kwao kupata kazi au kufanya biashara.

Hata wenyeji walipotwaa biashara zilizomilikiwa na raia wa Asia, kulikuwa na mkanganyiko kuhusu biashara kwa kuwa wenyeji wengi hawakuwa wameamua kuhusu walichokuwa wakitaka kufanya kutoka kwa nafasi nyingi zilizokuwepo.

Francis Macharia, Mwenyekiti wa Kitaifa wa Chama cha Wafanyabiashara, alieleza wazi miaka ya 1960: "Waafrika wengi wamechanganyikiwa kabisa. Hawajui wafanye biashara au kulima au kitu kingine - na kuna tabia ya kuchukulia biashara kama kitu cha kupitisha muda."

Kupanda kwa Rishi Sunak kuwa Waziri Mkuu wa Uingereza ni sawa na hadithi nzuri iliyoanzia kwa kukataliwa kisiasa katika Afrika Mashariki.

***jkamau@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# Waziri Mkuu mpya atatiza hali ya siasa

● NA OMULO OKOTH

Kupanda kwa Rishi Sunak hadi kileleni cha uongozi kunafufua kumbukumbu za kununuliwa kwa kampuni ya Land Rover na kampuni ya Tata Motors mnamo 2008.

Majarida yasiyojali ya Uingereza yampende yasimpende, na kukubali hali ilivyo, atakuwa akiishi No. 10 Downing Street, mojawapo ya ofisi za kifahari ulimwenguni.

Akiwa mzaliwa wa wazazi Wahindi, kupanda cheo kwa Sunak hadi kuwa kiongozi wa chama cha Conservative kunaweza kubashiriwa kama kupangua mpangilio wa kisiasa na kijamii nchini Uingereza.

Lakini mbali na joto ambalo kupanda kisiasa kwa Sunak kunazua, uwezekano (wa koloni kutwaa ufalme) dalili zilianza kuonekana wakati Land Rover, kampuni kubwa ya Uingereza iliponunuliwa na kampuni ya India mnamo 2008. Kubadilika kwa umiliki kulizua ubishi katika mpangilio wa kibiashara, kijamii na kitamaduni nchini Uingereza.

"Je, tunawezaje kupoteza Land Rover, na zaidi kwa nchi ya Asia, kwa koloni?" maswali kama hayo yalitawala mijadala ya kijamii Uingereza habari zilipotokea kwamba gari lililohusishwa na nguvu za Uingereza ulimwenguni na ufanisi wa uchumi, liliuziwa kampuni kubwa ya India.

Hata Kenya, ambako Land Rover ilihusishwa na nguvu za serikali, habari hizo zilitamausha watu wengi wa kawaida ambao chuki yao kwa chochote kutoka India ilianza enzi za kikoloni.

Hawakuweza kuamini masikio yao walipopata habari kwamba Tata Motors ilikuwa imenunua Land Rover na Range Rover.

Hali kwamba baba ya Sunak alizaliwa Kenya inaweza kuwa faraja ya kutosha, lakini maswali mengi yataulizwa.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group "ePaper Copy"

kurunzi ya kenya

UINGEREZA INATAKA KUIMARISHA UHUSIANO BAADA YA BREXIT

# JE, ATAPENDELEA AFRIKA?

*Ingawa msimamo wa Waziri Mkuu wa Uingereza kuhusu biashara haujabainika, viongozi wa Afrika wanatumai atalipa bara hili umakini unaohitajika akilinganishwa na watangulizi wake*

• Na LEVIN OPIYO

Wiki hii, Rishi Sunak amekuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Uingereza asiye Mwingereza asili na mchanga zaidi katika kipindi cha miaka 210 akiwa na umri wa miaka 42.

Mwanasiasa huyo wa chama cha Conservative, aliye na mizizi katika mataifa tofauti, sasa ana jukumu kubwa la kutoa Uingereza katika hali ngumu ya kiuchumi ya sasa ambayo imesababishwa na kutokuwa na hakika kisiasa na gharama ya riba.

Aliangazia haya katika hotuba yake ya kwanza nje ya ofisi yake ya 10 Downing Street, alisema: "Sasa hivi, nchi yetu inakumbwa na hali ngumu ya kiuchumi. Nitafanya imani ya uthabiti wa kiuchumi kuwa wajibu muhimu zaidi wa serikali hii."

Kwa kiwango kikubwa, Sunak, ni mwanachama sugu wa Conservative. Alizaliwa katika familia iliyojiweza na alisomea shule nzuri Uingereza. Winchester College, aliyosomea elimu ya upili, inatoza karo ya pauni 45,000 (karibu Sh6,300,000) kwa mwaka na imetoa zaidi ya mawaziri sita wa fedha nchini humo.

Baadaye alijiunga na Oxford kusomea filosofia na uchumi, kabla ya kuelekea Stanford, Amerika kusomea Digrii yake ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara (MBA).

Ni alipokuwa akifanya kazi katika Silicon Valley, California, baada ya kuhitimu MBA, ambapo alikutana na mkewe, Akshata Murthy, binti ya Narayana Murthy, bilionea anayemiliki Infosys, kampuni ya pili kwa ukubwa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano nchini India. Anamiliki asilimia 0.93 ya hisa katika kampuni hiyo na kumfanya mmoja wa wanawake tajiri zaidi nchini Uingereza.

Kwa wapigakura wa kawaida Uingereza, kutoka familia inayojiweza kunamaaniisha ni tajiri kiasi na haelewi maisha yao vyema. Hivyo basi, hawezi kuunda serikali itakayojali maslahi yao.

Katika video ya BBC mnamo 2001 iliyosambazwa Julai mwaka huu akifanya kampeni ya kuchukua nafasi ya Boris Johnson, Sunak alijigamba "nina marafiki wa familia za kifalme. Nina marafiki wa tabaka la juu," lakini hana marafiki wafanyakazi.

Wiki kadhaa baadaye, katika tamko la umma lililonuiwa kuwashawishi raia wa kawaida baada ya video hiyo ya kuaibisha, Sunak alisema katika mahojiano na runinga ya ITV: "Nikiwa na binti zangu, basi tukula 'the wrap'. Kauli yake hiyo iligeuka janga mkahawa wa McDonald uliposema uliacha kuuza chakula hicho 2020 na kuthibitisha tena hakuelewa maisha ya mwananchi wa kawaida.

Mapema mwaka huo, ripoti ziliibuka jinsi mkewe alikuwa akiomba hali spesheli ya ushuru, kumaanisha hakufaa kulipa Uingereza ushuru kwa pesa alizopata nje ya Uingereza.

Kulingana na Ronen Palan, Profesa wa siasa za Kimataifa katika Chuo Kikuu cha City of London, " sheria za ushuru zinaweza kutumiwa, au wakati mwingine kutumiwa vibaya na wageni au raia wa Uingereza kuepuka kulipa kodi." Haya yalitendeka wakati ambao mumewe alikuwa akiongeza ushuru akiwa waziri wa fedha, na kulaumiwa vikali, hali iliyoathiri vibaya azma yake ya kisiasa.

Halikuwa jambo la kushangaza basi ali-

...Endelea Uk 9



Waziri Mkuu mpya wa Uingereza, Rishi Sunak, akitoa hotuba nje ya ofisi yake, No. 10 Downing Street, katikati mwa jiji la London, mnamo Oktoba 25.

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ KASI YA KUCHIMBA MAFUTA ILIPUNGUA KUTOKANA NA KUSHUKA KWA BEI DUNIANI

# MAFUTA: NDOTO AU UKWELI?

*Awamu ifuatayo inahusu uchimbaji, usafishaji na usafirishahi kupitia kwa bomba, Na kazi hiyo inahitaji pesa nyingi na zaidi ya ujuzi wa kutafuta mafuta tu. Ilivyo sasa, haijabainika kuhusu iwapo kampuni ya Tullow PLC itaendelea na mradi huo, itatafuta mshirika au itauuza kwa kampuni nyingine*



● NA ROBERT SHAW

Shughuli ya uchimbaji mafuta katika eneo la Turkana nchini Kenya ni hadithi ndefu ambayo bado haijaonyesha mafanikio yoyote ya kifedha, kama vile mapipa yanayouzwa kwa siku. Hata hivyo, huenda juhudi hizo hatimaye zikaanza kuonyesha matokeo mazuri.

Kiwango kikubwa cha mafuta kiligunduliwa miaka kumi iliyopita katika eneo la Kaskazini mwa Kenya.

Tullow Oil ndiyo kampuni kuu ambayo imekuwa ikiendesha juhudi za kuchimba mafuta Kenya. Sawa na miradi mingine mingi kama huo, mafanikio yake yamekuwa yakihusishwa na gharama ya uchimbaji na bei za mafuta ulimwenguni.

Uchimbaji mafuta ni shughuli ghali sana inayotumia pesa nyingi na hatimaye huathiriwa na bei zilizopo ulimwenguni. Kuhusu Kenya, kuna kazi ya kuchimba mafuta hayo na kuyasafirisha umbali wa mamia ya kilomita.

Tullow Oil inamiliki asilimia 50 katika maeneo ya kuchimba mafuta ya 10BA, 10BB, 13T na asilimia 100 katika 12BB. Imekuwa ikiendesha shughuli za kutafuta na kuchimba tangu 2012.

Eneo la mafuta likiwa mbali, kaskazini mwa Turkana, inamaanisha mafuta yoyote yatahitaji kusafirishwa kwa bomba kilomita 825 hadi katika jijini Lamu, eneo la Pwani.

Hiyo ina maana kuwa, ando na gharama ya uzalishaji, ambayo



Eneo la mafuta la Ngamia 3 katika kijiji cha Nakukulas, Kaunti Ndogo ya Turkana Kusini.
PICHA | MAKTABA

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya




**Eneo la mafuta la Ngamia 8, Lokichar, Kaunti Ndogo ya Turkana Kusini.** JARED NYATAYA I NATION

ni karibu dola za Amerika 22 (Sh2,600) kwa pipa moja, ni lazima iongezwe gharama ya usafirishaji hadi Lamu. Usafirishaji wake ni jambo linalohitaji pesa nyingi pia.

Inakisiwa kuwa huenda vipande hivyo vikazalisha karibu mapipa 120,000 kwa siku kwa muda wa miaka 23.

Shughuli za uchimbaji zilipunguzwa kutokana na kushuka kwa bei za mafuta duniani. Bei za mafuta zimekuwa kati ya Sh4,800 na Sh7,200 kwa pipa moja kati ya 2011 na 2021. Kwa sasa, pipa moja linauzwa kwa kati ya Sh13,000 na Sh14,000. Si vigumu kuona uhusiano kati ya kupungua kwa shughuli za uchimbaji na kushuka kwa bei ya mafuta.

Kutokana na kupanda kwa bei, shughuli za uchimbaji zimeanza kuongezeka. Kuna dhana kuwa hata bei za zikishuka tena, hazitafikia kiwango kilichoshuhudiwa katika mwongo mmoja uliopita.

Tullow ilikuwa tsysri imetumia Sh120 bilioni kutambua maeneo yaliyo na mafuta. Mnamo Januari, ilikisiwa ingehitaji Sh600 bilioni inapoelekea katika awamu nyingine ya kuchimba na kusafirisha mafuta ya kuuza. Hizo zinajumuisha Sh400 bilioni za uchimbaji na uzalishaji.

Kinachoibuka ni kuwa ufanisi mkuu wa Tullow ni katika kutafuta mafuta na kuyachimba.

Hata hivyo, ikifikia utekelezaji wa masuala muhimu kama miundomsingi na uuzaji, huwa inatafuta mashirika mengine.

Mnamo Agosti, kulikuwa na mazungumzo yaliyozishirikisha kampuni mbili kutoka India - ONGC Videsh na Indian Oil Co - kuhusu mkakati wa kuwekeza katika maeneo ya kuchimbia mafuta. Lengo kuu ni kuhakikisha mafuta yanachimbwa, kusafirishwa, kusafishwa na hatimaye kuuzwa.

Haijabainika kuhusu iwapo mazungumzo hayo yamezaa matunda yoyote, lakini kilicho wazi ni kuwa mazingira ya kibiashara ya kuboresha visima vya mafuta eneo la Turkana yameimarika. Kile kinachohitajika ni mwekezaji au mshirika mwenye uwezo mkubwa kifedha, ili kuupeleka mradi huo katika hatua nyingine.

Suala lingine ambalo limechelewesha shughuli hiyo ni muda ambao serikali na Wizara ya Kawi imechukua kuipa Tullow leseni zinazohitajika za kuzalisha mafuta.

Hilo linazua malalamishi ambayo yamekuwepo kuwa, ingawa serikali hutamani sana uwekezaji mkubwa, mara nyingi ndiyo huwa kikwazo kikuu.

Kulingana na hali ilivyo sasa, haijabainika kuhusu iwapo kampuni ya Tullow PLC itaendelea na mradi huo, itataka mshirika au itauuza kwa kampuni nyingine.

Ikizingatiwa uwezo wake mkubwa uko katika uchimbaji, swali ni kuhusu jinsi na yule itakayeshirikiana naye kutekeleza awamu ifuatayo. Awamu hiyo inajumuisha utengenezaji na uendeshaji wa bomba la kilomita 825 hadi Lamu.

Matumaini kuhusu mafanikio ya kifedha ya mafuta yameimarika katika eneo hilo, ikiwa bei za sasa duniani zitaendelea kubaki zilivyo.

Swali ni kwamba awamu ifuatayo inahusu uchimbaji, usafishaji na usafirishaji kwa bomba, kazi ambayo inahitaji uwekezaji mkubwa wa kifedha, kuliko tu mbinu za kutafuta mafuta.

***Robert Shaw ni mchanganuzi wa masuala ya sera ya umma na uchumi: robshaw298@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# Matumaini Afrika baada ya Rishi kutwaa uongozi

...Kutoka Uk 7

poshindwa na Liz Truss, ambaye hakuwa maarufu zaidi katika uchaguzi wa kumrithi Boris Johnson. Alitoweka katika ulingo wa siasa, na kuacha wengi wakibahatisha hatua aliyopanga kuchukua, bahati ilipomwangukia.

Uamuzi wa Truss wa kuchochea uchumi kwa kukopa mabilioni ili kupunguza ushuru ulitumbukiza nchi katika hatari kubwa wa kiuchumi, na kumfanya ajiuzulu. Katika hali hiyo, Sunak alikuwa mtu aliyefaa, si kwa sababu alikuwa wa pili katika uchaguzi wa kumrithi Johnson lakini kwa sababu ya wadhifa wake wa awali kama Waziri wa Fedha. Akiwa Waziri, alisifiwa kwa sababu ya mpango wake ambao ulikuwa umeokoa biashara nyingi, kazi, na familia wakati wa janga.

Kwa upande mwingine, alikuwa amezima viwango vyote vya ushuru, na kufanya watu kulipa ushuru wa juu. Ripoti iliyotolewa mwaka huu na Afisi ya Mapato na Forodha ilionyesha kuwa idadi ya watu waliokuwa wakilipa asilimia 40 au asilimia 45 ya ushuru waliongezeka kutoka 4.25 milioni hadi 6.1 milioni.

Ingawa hajataja hadharani jinsi akiwa Waziri Mkuu atatatua hali ya sasa ya uchumi, kuna uwezekano atatumia mbinu sawa, kupunguza matumizi na kuongeza ushuru. Kwa kufanya hivi, atatekeleza manifesto ya chama chake ambayo inashikilia kupunguzwa kwa matumizi.

Hii pia itamsaidia kuepuka kujipata katika hali sawa na mtangulizi wake, ambaye alienda kinyume na manifesto na matokeo yakawa mabaya.

Katika kiwango cha kimataifa, msimamo wake katika biashara, usalama na maendeleo haujabainika. Baadhi, hasa katika Afrika, wanatumai atalipa bara hili umakini unaohitajika akilinganishwa na watangulizi wake.

Kabla ya Theresa May kuzuru Afrika mnamo 2018, uhusiano wa Uingereza na Afrika ulikuwa ukiendelea kufifia tangu vita baridi vilipoisha. Ziara hiyo ilisababishwa na Brexit, ambayo ilimlazimisha kutafuta uhusiano na nchi zilizopuuzwa na miungano mipya huku Uingereza ikijiandaa kujiondoa katika Muungano wa Ulaya.

Johnson alikuwa ametembelea bara la Afrika akivumisha umuhimu wake kimikakati. Hata hivyo, alipomrithi May kama Waziri Mkuu, aliangazia zaidi kuondoa Uingereza katika EU, huku akichukua hatua za kupunguza msaada kwa Afrika. Baada ya msururu wa kashfa yeye pia alilazimishwa kujiuzulu.

Ingawa ni kweli baba ya Sunak alizaliwa Kenya, kwa sasa atashughulika zaidi na masuala ya nchi yake, Uingereza. Kando na hali ngumu ya kiuchumi, kuna vita vinavyotokota ndani ya chama cha Conservative ambavyo atahitaji kutatua iwapo kitakuwa na nafasi ya kushinda katika uchaguzi mkuu ujao.

Hata hivyo, Uingereza imekuwa ikitia saini mikataba mipya ya kibiashara na nchi za Afrika ikitafuta mahusiano mapya na kuimarisha ya zamani baada ya Brexit.

Kulingana na Patrick Smith, Mhariri Mkuu Msimamizi wa jarida la Africa Report, huenda msimamo wa Sunak kuhusu Afrika utabainika katika kongamano la G20 jijini Bali, ambako Muungano wa Afrika, ukisaidiwa na China, utashinikiza kujumuishwa katika kundi hilo.

Pia kutakuwa na taarifa kutoka kwa mashirika kadhaa kama Benki ya Maendeleo ya Afrika na IMF kwa mataifa yenye nguvu ulimwenguni kuweka mpango wa kuondolea madeni nchi zinazoendelea.

***Mwandishi ni mwanahabari na mtafiti Mkenya anayeishi London.***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

MAAFISA HARAMU



# WALIPEWA LESENI YA KUUA

*Operesheni za vikosi maalumu vya polisi ziliibua maswali kufuatia madai kuwa wanachama wake walihusika katika mauaji ya kiholela badala ya kupambana na uhalifu.*

Nation Media Group "ePaper Copy"

● NA DOMINIC WABALA

Mnamo Januari 27, 2005, mmoja wa majambazi hatari nchini aliuawa kwa kupigwa risasi katika maficho yake, mtaa wa Zimmerman, Nairobi, baada ya makabiliano ya saa tano.

Shughuli za uhalifu za aliyekuwa polisi, Daniel Kiptum Cheruiyot, ambaye alikuwa ameua polisi wawili, zilifikia kikomo katika operesheni iliyoongozwa na aliyekuwa Kamishna wa Polisi Meja-Jenerali Mohammed Hussein Ali na aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai (DCI) Joseph Kamau.


Cheruiyot aliuawa na mseto wa maafisa kutoka vikosi vya Flying Squard na Kanga Squad.

Wakati wa makabiliano hayo, polisi walirusha vitoa machozi ndani ya nyumba yake na risasi nyingi. Lakini naye aliendelea kuwafyatulia risasi maafisa hao. Mwishowe alitoka nje na bunduki yake aina ya Uzi, iliyotengenezwa nchini Israeli. Kosa kubwa. Afisa mmoja alimpiga risasi kichwani na akafa papo hapo.

Kikosi cha Flying Squad wakati huo kiliongozwa na Musa Yego ilhali kile cha Kanga kilikuwa chini ya uongozi wa George Kinoti, ambaye baadaye alipanda cheo kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI).

Vikosi hivi viwili ni miongoni mwa vingi maalumu vya polisi vilivyobuniwa miaka ya nyuma kupambana na uhalifu, hasa ulanguzi wa mihadarati, wizi katika benki na wizi wa magari.

Hata hivyo, operesheni za vikosi hivyo ziliwekwa kwenye darubini kufuatia madai kuwa maafisa wake walihusika katika mauaji ya kiholela badala ya kupambana na uhalifu.



**Aliyekuwa Kamisha wa Polisi Meja Jenerali Mohammed Hussein Ali (katikati) na mkurugenzi wa DCI wakati huo, Joseph Kamau (nyuma yake) wakiongoza maafisa wengine kusaka majambazi waliopiga risasi na kuua polisi wawili katika mtaa wa mabanda wa Lunga Lunga Nairobi, mnamo Aprili 22, 2004.**
PICHA | MAKTABA

Rais William Ruto alipoingia mamlakani, aliamuru kuvunjwa kwa Kikosi cha Huduma Maalumu cha DCI (SSU) kutokana na madai kuwa maafisa wake walihusika katika kutoweka kwa watu kwa njia za kutatanisha.

Katika miaka ya 1990 gari aina ya Peugeot 504 lilipoonekana mtaani au katika kituo cha biashara, wanaume wote wangetoroka. Aliyekamatwa na kuweka kwenye buti la gari hilo, lililoendeshwa kwa kasi, angeuawa au kujipata gerezani.

Waliopitia mateso ya maafisa hao hawakuishi kuelezea masaibu yao, na kama waliweza kuishi, maisha yao yalivurugwa kabisa.

Kikosi cha Flying Squad kilitambuliwa kwa ukatili wake, kiliendesha shughuli zake kinyume cha sheria. Maafisa wake wa vyeo vya chini walikiuka Kanuni za Polisi kwa kuwapuuza maafisa wakuu na kuwajibika moja kwa moja kwa mkuu wa DCI.

Kando na Flying Squad na Kanga, kulikuwa pia na Kwekwe, Eagle, Rhino, Novemba na Spider.

Kikosi cha Flying Squad kilianzishwa na aliyekuwa Mkurugenzi wa DCI, Noah arap Too, kupambana na wezi wa magari, wezi wa benki, wezi wa maduka na majambazi wengine.

Kiliongozwa na maafisa wawili wa cheo cha Inspekta Mkuu, Timothy Kamunde na Daniel Seroney. Kamunde mara nyingi alijitambualisha kwa jina lake na kuongezea cheo chake (Timothy Kamunde, Inspekta Mkuu).

Angempa mshukiwa gari la polisi lisilo na nambari kuwaleta washirika wake na mshukiwa angefanya hivyo. Ndani ya gari lake, Kamunde alibeba vipande vya vyuma, mapanga, kamba na bunduki. Inasemekana alipendelea kutesa washukiwa; mara nyingi hakutumia bunduki.

Wakati mmoja akitoa ushahidi katika Mahakama ya Nakuru, Kamunde alitolewa kijasho na mshukiwa kwa maswali magumu. Akiwa mbele ya hakimu, Kamunde alimuonya mshukiwa huyo arudie maswali hayo nje ya mahakama. Mshukiwa alikataa kutoka mahakamani na akamuomba hakimu ampe ulinzi.

Kamunde aliogopewa hata na maafisa wa ngazi za juu ambao

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## Waliokuwa wakuu wa kikosi cha Flying Squad


Munga Nyale


Musa Yego


Francis Njiru


Francis Okonya

## Waliokuwa wakuu wa DCI


Francis Sang


Joseph Kamau


Noah arap Too

George Kinoti aliongoza kikosi cha Kanga Squad na baadaye akaunda Kikosi cha Huduma Maalumu (SSU) akiwa mkuu wa DCI.



hakuwa chini yao. Baada ya kustaafu, wakati mmoja alirudishwa kazini na Rais Daniel arap Moi kusaidia kukomesha wizi wa mabavu. Alipewa mamlaka makuu na aliwajibika tu kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upelelezi wa Jinai (DCI). Hata maafisa waliokuwa na vyeo vya juu kumzidi walikuwa wakiripoti kwake.

Wakati wa kuvunjwa kwa Flying Squad, ilisemekana baadhi ya maafisa walipatikana na zaidi injini tano za magari yaliyoibwa na walishukiwa kuwa washirika wa majambazi wenye silaha.

Ili kukabiliana na kikosi katili cha Flying Squad, mkurugenzi wa DCI wakati huo, Francis Sang alibuni Kikosi Maalumu Cha Kuzuia Uhalifu (SCPU) mnamo 1999, kikiongozwa na Peter Kavila. Kikosi hicho kilishirikisha makamanda waliosajiliwa kutoka kitengo cha kupambana na fujo (GSU).

Kilipewa kazi ya kuzuia wizi wa kutumia silaha, ulanguzi wa mihadarati na binadamu, wizi wa bidhaa zinazosafirishwa na wizi wa benki. Flying Squad iliendelea na shughuli zake ingawa kwa kiwango cha chini, ikiongozwa naSammy Githui, Francis Okonya, Sebastian Ndaru, Munga Nyale, Musa Yego na Said Kiprono.

Yego, mlenga shabaha stadi, alisimamia kikosi cha Flying Squad kwa miaka kadhaa hadi alipopandishwa cheo kuwa Afisa wa Upelelezi wa Jinai katika Mkoa wa Kaskazini Mashariki.

Katika kitabu chake cha kumbukumbu, Sang alisema kuwa, kutokana na changamoto za kijamii na kiuchumi kama vile umasikini na watu kuhamia mijini, visa vya wizi wa magari, wizi wa benki na wizi wa maduka viliongezeka wakati wa hatamu yake.

Kisha kulikuwa na Kwekwe, kikosi kilichoundwa kupambana na kundi haramu la Mungiki ambalo lilikuwa limehangaisha Wakenya kwa muda mrefu. Kiliongozwa na Inspekta Mkuu Zebedio Maina.

Maina alikuwa mkatili kiasi kwamba yeyote aliyedhaniwa kuwa mfuasi wa Munguki aliamua kuhama la sivyo angekiona cha mtema kuni. Alipendelea kufanya kazi pekee yake au na maafisa wachache aliowaamini.

Kufuatia malalamishi ya umma, Kwekwe kilibadilishwa jina kuwa Eagle na shughuli zake zikahamishwa hadi Kituo cha Polisi cha Buruburu.

Baada ya Kavila kuondoka SCPU, kiliwekwa chini ya uongozi wa Richard Katola, aliyepata umaarufu kwa kukomesha wizi wa pesa zilizokuwa zikisafirishwa na kampuni ya ulinzi ya G4S. Kikosi hicho kilikomboa sehemu ya mamilioni ya pesa zilizoibwa na wafanyakazi wa G4S na kuzima mtindo huo wa wizi.

Katola alishiriki katika operesheni dhidi ya Mungiki kati ya 2007 na 2012 wakati ambao kikosi hicho kililaumiwa kwa mauaji ya kiholela ya wafuasi wa kundi hilo haramu. Aliugua kwa miaka mitano kabla ya kufa Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta. Maina, Kariuki na mkuu mwingine wa Flying Squad, Reche Nyaga pia walifariki kwa njia tatanishi. Maafisa wengi wa kikosi hicho pia wamepotea na hawajulikani waliko. Benard Kiriinya dereva wa kikosi hicho, aliyeungama kupitia kwa video kuwa alishiriki mauaji ya kiholela na aliyetarajiwa kutoa ushahidi kortini, alipigwa risasi na kuuawa na wenzake katika mtaa wa Westlands, Nairobi, 2010. Hiyo ni licha ya kuwa alikuwa amepewa makao salama na Tume ya Kutetea Haki za Binadamu.


Aliyekuwa mkuu wa SCPU, Peter Kavila

Kikosi cha SCPU kilitambuliwa kwa kazi yake. Mnamo 2010, gari aina ya Toyota Prado lililoibwa lilipatikana Taveta na makachero wanne waliotumwa kulichukua walimleta mshukiwa waliyempata nalo na washirika wake wanne waliokamatwa maeneo ya Mwatate, Voi, Athi River na Mlolongo. Mshukiwa aligongwa kwa chupa ya soda ndipo akapeleka makachero hao walikokuwa wamejificha wenzake.

Baadaye kulikuwa na kikosi cha Track Unit kilichoshirikiana na Kitengo cha Ujasusi wa Jinai (CIU) na SCPU, kilichobadilishwa jina kuwa Kikosi cha Huduma Maalumu (SSU) baada ya Kinoti kuwa Mkurugenzi wa DCI na kuvunja Flying Squad.

Kikosi cha Track Unit kilichokuwa na makao yake eneo la Parklands, kikiongozwa na Francis Njiru, kiliundwa kusaidian SCPU na CIU kufuatilia kesi za vikosi hivyo viwili na kuzuia ushahidi kupotea.

Kanga Squad kilihusika katika kesi nyingi, ukiwemo uchunguzi wa kesi ya wizi dhidi ya mwandishi Ngugi Wa Thiong'o na mkewe chumbani mwao katika hoteli ya Norfolk. Kilivunjwa baada Kamau kuondolewa kama mkurugenzi wa DCI na maafisa wake wakatumwa katika vituo mbalimbali vya polisi.

Baada ya kuteuliwa mkurugenzi wa DCI, Kinoti aliunda upya Kanga Squad na kupeleka maafisa wake katika ofisi za DCI Parklands. Waliripoti kwake (Kinoti) na kutekeleza majukumu maalumu kama vile operesheni dhidi ya bidhaa ghushi kama sukari, mchele, mafuta ya kupikia na uagizaji magurudumu nchini. Kitengo hicho kilifanya kazi chini ya asasi mbalimbali za serikali ikiwemo Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru (KRA), DCI na Shirika la Kukadiria Ubora wa Bidhaa Nchini (KEBS).


Mapema mwezi huu, IPOA ilitangaza kuwa inachunguza malalamshi kadhaa ya mauaji ya kiholela yaliyotekelezwa na polisi. "Kwa mujibu wa sehemu 4, 5, 6, na 7 za Sheria ya IPOA, mamlaka hii imeanzisha uchunguzi na ukaguzi wa kikosi kilichovunjwa juzi cha SSU na vikosi vingine ndani ya Huduma ya Kitaifa ya Polisi (NPS) ili kubaini kiwango cha utendakazi wake na kiwango chake cha utaalamu. IPOA pia inachunguza vitendo vya NPS kufuatia malalamishi kadhaa kuhusu kupotea kwa watu, utekaji nyara na mauaji," mwenyekiti wa IPOA, Anne Makori akasema kwenye taarifa.

Mnamo Januari mwaka huu, IPOA ilianza kuchunguza kisa ambapo miili 25 ilipatikana katika mto Yala. Mkurugenzi wa shirika la kutetea haki, Amnesty International Kenya, Irungu Houghton, ametoa wito kwa NPS ichunguze kikosi kilichovunjwa cha SSU kuhusu mauaji ya kiholela.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



Mfanyakazi akiweka vizuri mchoro wa Bernardo Cavallino wa *Saint Bartholomew* katika Sotheby mnamo Oktoba 25. PICHA | AFP




Mfanyakazi wa kampuni ya Kenya Airways akidhibiti chombo cha angani kisichoendeshwa na mtu (UAV) kunyunyiza dawa katika Shamba la Chai la Kipkebe, eneo la Musereita mnamo Oktoba 21. PICHA | AFP



Mwanaume akishiriki maandamano ya kupinga mkataba wa maelewano kati ya Italy na Libya jijini Rome mnamo Oktoba 26. PICHA | AFP



Wanawake wa jamii ya Turkana wakiketi na watoto wao chini ya kibanda cha kukinga jua wakati wa hafla ya kusaidia jamii zinazoathiriwa na Ukame iliyoandaliwa na Hazina ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Elimu ya Watoto katika kijiji cha Nadoto mnamo Oktoba 18. PICHA | AFP



Msichana akilala katika ufuo wa bahari eneo la Karachi, Pakistani, mnamo Oktoba 25. Wazazi wake wanaamini akipigwa na jua atapona ugonjwa anaougua. PICHA | AFP



Erling Haaland wa Manchester City akisherehekea baada ya kufunga bao dhidi ya timu ya Brighton wakati wa mechi ya Ligi Kuu katika Uwanja wa Michezo wa Etihad mnamo Oktoba 22. City walishinda 3-1. PICHA | AFP

Nation Media Group "ePaper Copy"

Jukwaa La

# Vijana



# ROBOTI NA BINADAMU

*Sekta ya robotiki inatarajiwa kukua kwa kiwango kikubwa miaka inayokuja. VENO Autobotics, kampuni ya Kenya, inataka kubadilisha Afrika badala ya mtumiaji wa teknolojia iwe mshirika mkuu katika sekta hiyo*

NAFASI YA VIJANA

# FUNGUA MACHO KWA ULIMWENGU DIJITALI

**MATANGAZO YA BIASHARA:** WhatsApp ilipozima kwa saa kadhaa kila mahali, mabilioni ya watu waliathirika ulimwenguni kote

● NA MUTHONI NJAKWE

Kwa saa kadhaa mnamo Jumanne, ulimwengu wa kidijitali nusura usimame baada ya mtandao wa kijamii wa WhatsApp, unaomilikiwa na kampuni ya huduma za kutuma jumbe ya Meta, kuzima kote duniani. Watumiaji wa mtandao huo waliripoti matatizo ya kutuma na kupokea jumbe. WhatsApp ilisema tatizo hilo lilisababishwa na hitilafu ya kiufundi.

"Tunajua watu walikumbwa na matatizo ya kutuma jumbe kupitia WhatsApp leo. Tumerekebisha suala hilo na tunaomba radhi," msemaji wa Meta akasema. WhatsApp imekuwa muundomsingi muhimu kwa masoko mengi huku ikitumiwa na mabilioni ya watu.



Kufikia 2020, huduma hiyo ilikuwa inatumiwa kutuma jumbe zaidi ya 100 bilioni kwa siku, idadi ambayo haina mshindani katika sekta hiyo.

Mitandao wa Facebook Messenger na WhatsApp kwa pamoja ilitumiwa kubadilishana jumbe 60 bilioni kwa siku kufikia mwanzoni mwa 2016. Hii inaashiria jinsi sekta ya digitali ilivyogeuka kuwa muhimu katika uendeshaji wa biashara kote duniani, hasa katika matangazo ya bidhaa.

Matangazo ya biashara kidijitali, kwa mfano, si jambo la kuwazia tena katika kizazi cha sasa cha kiteknolojia. Ulimwengu unavyozidi kuhamia enzi ya dijitali, litakuwa jambo la kawaida kwa biashara zote kuwa sehemu ya ulimwengu wa dijitali.

Mwongo mmoja uliopita, kutokana na mifumo ya kiasili, shughuli ya matangazo ya biashara ilikuwa jambo la fahari, yaliachiwa mashirika makubwa yenye bajeti kubwa za matangazo ya biashara. Teknolojia, hata hivyo, imebadilisha matangazo ya biashara: biashara za kila aina zilizo na bajeti za viwango tofauti sasa zinaweza kupigia debe bidhaa zake katika jukwaa moja.

Kupitia matangazo kidijitali, unaweza kufikia hadhira pana zaidi kuliko unavyoweza kupitia mbinu za kiasili. Aidha, ni nafuu zaidi kushinda matangazo ya biashara ya kiasili na hukuwezesha kupima ufanisi wako kila siku.

Hata hivyo, kabla ya kujitosa katika uundaji na usambazaji wa matini au kuzindua kampeni za matangazo ya biashara kidijitali, ni muhimu kuwa na mikakati madhubuti ya matangazo ya biashara kidijitali.

Kuorodhesha wazi malengo yako ndiyo hatua ya kwanza ya mafanikio katika matangazo ya biashara kidijitali. Mikakati utakayobuni ya matangazo ya biashara kidijitali itategemea maazimio yako. Kama azma yako ni kuongeza uhamasishaji wa bidhaa, huenda ukahitajika kutilia maanani zaidi kufikia hadhira mpya kupitia mitandao ya kijamii. Baada ya kuelezea bayana shabaha yako, hatua inayofuata ni kutambua hadhira unayolenga.

Kiambajengo kingine muhimu cha matangazo ya biashara kidijitali ni uundaji wa matini. Hakikisha matini unayobuni na kusambaza mitandaoni ina thamani, mwafaka na yenye mtiririko. Matini bora ndiyo tiketi yako ya kunasa umakinifu wa hadhira.

Mwisho, ili kubuni mikakati kabambe ya matangazo ya biashara kidijitali kwa muda mrefu, ni muhimu timu yako ijifunze jinsi ya kupata mwelekeo kutokana na takwimu kidijitali. Kwa kutumia nyenzo tofauti za takwimu kidijitali, unaweza kufuatilia kubaini iwapo unatimiza malengo yako au la.

Bi Njakwe ni mtaalamu wa matangazo ya biashara kidijitali na Afisa Mkuu Mtendaji wa Stedcomm, kampuni ya matangazo ya biashara kidijitali.

*Je, wewe ni kijana mwenye maono? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni na mtazamo wako kuhusu masuala ibuka kupitia:* ***weeklyreview@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

## WANAVYOSEMA



**Oluoch Akong'o**

Mauaji ya mwanahabari raia wa Pakistani Arshad Sharif hayakuwa ajali jinsi serikali ya Kenya inavyotaka tuamini. Ni kisa kingine cha ukiukaji wa haki za kibinadamu nchini. Mauaji ya kiholela yamekua suala sugu kwa muda mrefu. Vijana wengi kutoka jamii fukara na zilizotengwa wameuawa na polisi au vikosi vingine vya usalama. Ni lazima serikali iwafungulie mashtaka wahusika wa mauaji kiholela.

*— Kiongozi wa Wanafunzi, Chuo Kikuu cha Kenyatta (KU)*



**Allan Achieng'**

Polisi kila mara hufuata maagizo ya wakubwa wao. Ni mikakati gani imebuniwa kukomesha ukatili wa polisi? Je, inamaanisha mtu anaweza kufyatua risasi tu kiholela wakati hakuna hatari? Pengine wangelenga magurudumu au wafuate gari hilo. Aina hii ya ukatili huwa tu inawaharibia polisi jina. Ni lazima serikali ikomeshe ukatili huu.

*— Rais, Chuo Kikuu cha Pwani*



**Lucia Atieno**

Inavunja moyo kwa mwanahabari kupoteza maisha yake kutokana na utepetevu licha ya kuwepo mikakati yote ya kulinda maisha ya watu wasio na hatia. Kwani hakuna sheria thabiti kuhusu mfumo na kanuni zinazotumiwa kushughulikia visa kama hivyo? Kama taifa, ni lazima tujirekebishe na kuchukua hatua bora inapohusu masuala ya sheria. Mambo yanaenda vibaya.

*— Mfanyabiashara*



**Rachel Koome**

Inasikitisha kuwa watu tunaotarajia watulinde ndio wanaotuua. Inahuzunisha kwamba kuna watu katika kikosi cha polisi wanaofanya kinyume kabisa na yanayotarajiwa kutoka kwao. Kuna mfumo wa sheria ya kukabiliana na washukiwa. Hatuwezi kuruhusu vitendo kama hivyo vya kinyama. Serikali inapaswa kuingilia kati na kuwalinda watu wake kutokana na maafisa wahalifu.

*— Mhudumu wa Kijamii*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

MTAZAMO WANGU

# HUDUMA YA POLISI NCHINI IREKEBISHWE



**Opereresheni:** Polisi wa Kenya daima huwa haelewi masilahi ya umma na hivyo hafai kutekeleza wajibu wa kudumisha usalama.

• NA WAGA ODONGO

Siku moja miaka mingi iliyopita, tukiwa matembezi usiku tulipotea. Tulikuwa mjini Nakuru, ambao siufahamu vizuri, na tulikuwa tukielekea klabu fulani.

Hii ilikuwa kabla ya kuanzishwa kwa apu za kuita teksi na hivyo ilitulazimu kuuliza ili tuelekezwe tulikokuwa tukinuia kwenda. Marafiki zangu wawili waliibua wazo: Mbona tusiulize afisa wa polisi?

Kuna mmoja aliyekuwa amesimama karibu na kituo cha petroli huku amevalia kabuti jeusi na kubeba bunduki.

Walimkaribia afisa huyo wa polisi na kuanza kuongea naye, hatua iliyotushangaza.

Sasa sina haja ya kukuambia kuwa marafiki zangu walikuwa raia wa kigeni, ni kweli?

Hawajui jinsi mambo yalivyo hapa Kenya. Hakuna Mkenya aliyepotea anaweza kuuliza afisa wa polisi amuonyesha anakotaka kwenda.

Polisi ni watu wa kuepukwa, ikiwezekana, na kuvumiliwa ikibidi. Ni mgeni pekee anayeweza kumuona polisi aliyebeba bunduki, akishika doria usiku, na asiingiwe na woga au kushikilia kwa nguvu kibeti chake.

Kwanza, nafahamu kuwa kazi ya polisi ni mojawapo ya kazi hatari nchini Kenya.

Mwaka jana, zaidi ya maafisa 100 wa polisi waliuawa, kulingana na takwimu rasmi.

(Ripoti hiyo haijatenganisha maafisa waliojiua na waliouawa wakiwa kazini). Polisi pia hufanya kazi katika mazingira magumu, kwa mishahara duni. Ni kazi isiyothaminiwa.

Kuvunjwa kwa Kikosi cha Huduma Maalumu, katika Idara ya Upelelezi wa Jinai cha kupambana na wahalifu (SSU) na kukamatwa kwa wanachama wa kikosi hicho walioshukiwa kuhusika na mauaji ya kiholela hakutoshi.

Huduma nzima ya polisi inafaa kufanyiwa marekebisho. Asasi hii bado haijathaminiwa na jamii kwa sababu haijajitenga na mizizi yake ya kikoloni. Ripoti ya 2009 ya Jopokazi la Kitaifa Kuhusu Mageuzi katika Polisi ilitaja huduma hiyo kama "kikosi cha kudhibiti raia", kilichobuniwa kuwalinda walowezi wa kikoloni kutokana na uhalifu uliodhaniwa kutoka kwa Waafrika."



Maafisa wa polisi katika doaria jijini Nairobi, mnamo Mei 7, 2020.

Leo hii dhana hiyo ingali inahusishwa na polisi hata kama wamevalia sare mpya.

Sote tuna masimulizi ya kibinafisi kuhusu visa vya ukiukaji wa haki vinavyotekelezwa na polisi.

Mnamo 2017, nilishiriki utayarishaji wa ripoti ya shirika moja lisilo la kiserikali kuhusu waathiriwa wa ukatili wa polisi. Nilifanya kazi kwa karibu na makao makuu ya polisi katika jumba la Vigilance.

Niliona mwili uliotolewa katika Ziwa Victoria ukiwa na kile kilichofanana na tundu za risasi.

Mwili wa mtu mwenye umri wa miaka 16 aliyeuawa kwa kupigwa rungu katika eneo la Sega, Kaunti ya Siaya (marungu ni bora kuliko bunduki kwa sababu hayaachi maganda), nilikutana pia na familia ya mwendeshaji bodaboda kwa jina Zachary Otieno, ambaye aliuawa kwa kupigwa risasi na kumuacha mkewe akiwa mja mzito. Familia yake haingepata Sh10,000 zilizohitajika kugharamia upasuaji wa maiti kuthibitisha kuwa mwanamume huyo aliauawa kwa risasi.

Mamlaka ya Kuchunguza Utendakazi wa Polisi (IPOA) haingeanza kuchunguza kisa hicho kwa sababu hapakuwa na ripoti kuhusu upasuaji wa mwili. Familia nyingi hulazimika kukopa pesa ili kugharamia upasuaji wa maiti, shughuli ambayo mara nyingi ripoti zake hazisaidii kufanikisha kushtakiwa kwa watekelezaji wa mauaji hayo.

Hata wanapoonekana wazi wakiua mtu kwa kumpiga risasi, hakuna hatua inayochukuliwa. Huwezi kuamini ulichoona kwa macho yako. Eric Kirui alikamatwa kwa kuwapiga risasi na kuwaua waandamanaji wawili wakati wa uchaguzi mku wa 2007 lakini kesi hiyo iliporomoka kwa kukosa ushahidi.

Sheria zote zimewekwa kuwasiadia polisi kukusanya pesa za hongo kutoka kwa raia. Kifaa cha kutambua madereva walevi cha alcoblow kiliwafaidi sana polisi.

Wakati mmoja karibu nigongwe na gari lililokuwa likiendeshwa, upande usiofaa, katika barabara kuu ya Thika Ijumaa jioni. Ni kana kwamba dereva alikuwa ametumia dawa fulani ya kulevya. Mita chache mbele yetu, niligundua kiini cha wendawazimu wake kilikuwa kizuizi cha polisi waliokuwa na alcoblow.

Polisi pia walitumia kafyu ya kudhibiti kusambaa kwa Covid-19 kama njia ya kujitajirisha. Ukaguzi uliofanyiwa polisi ulifichua jinsi maafisa wa vyeo vya juu walivyo katika biashara kubwa wakiweka akiba ya mamilioni ya pesa kila wiki. Kwao, kazi ya polisi ni kama ya ziada tu.

Polisi wa Kenya daima huwa haelewi masilahi ya umma na hafai kutekeleza wajibu wa kulinda usalama. Kufuatia mauaji ya raia wa kigeni wenye ushawishi, serikali hulazimika kujifanya imeshtuka huku ikichukua hatua kana kwamba mauaji ya kiholela ni kitendo kigeni.

Nadhani huduma nzima ya polisi inafaa kulaumiwa kwa sababu ya kuendeleza njama ya kuficha ukweli.

Leo kuna miili kadhaa iliyopatikana katika mito, maiti zilizoliwa na wanyama misituni na hakuna polisi aliyejitokeza kuelezea chanzo cha matukio kama hayo. Polisi wengi wamenyamaza wenzao wanapofanya makosa.

Polisi akifanya makosa, wenzake humtetea hata kama itabidi wavunje sheria. Kwa hivyo, si sawa kudai eti ni maafisa wachache wa polisi walio wabaya, uozo umeanzia kwa wenye vyeo vya juu hadi kwa wa vyeo vya chini.

*Bw Odongo ni Mhandishi wa Programu za Kompyuta*


*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

UVUMBUZI WA KITEKNOLOJIA

# ROBOTI ZAVAMIA BIASHARA

**BIASHARA YA MASHINI:** VENO Autobotics imeunda mifumo ya maziwa, mifumo ya malipo na inaendelea kuunda mfumo wa uegeshaji magari unaohusu kuweka vifaa vya kutambua hali ilivyo katika majumba ya kibiashara na maegesho



Victor Boit wa kampuni ya Veno Autobotics jijini Nairobi, Oktoba 27. PICHA | JEFF ANGOTE

• NA EDDY ASHIOYA

Kama kuna kitu kambacho Victor Boit anajutia ni kuwa hajawahi kufungua TV ya mama yake. Au ni DVD? Alizoea. Ni Maikrowevu? Amewahi. Redio je? Mara nyingi. Kwa hakika, sema redio mbili.

Sababu pekee ya kutofungua televisheni si kwa kuwa hakutaka kufanya hivyo, lakini ni kwa sababu hawakuwa na moja kwa muda mrefu. "Tulinunua TV tumechelewa," ananiambia tukizungumzia safari yake ya uhandisi. Haonekani kuwa fundi wa kawaida, unajua, yule aliye na miwani kubwa, nywele isiyotunzwa na kuvalia fulana ndefu yenye kofia.

Unaweza kudhani ni mtu wa kawaida kama si hali ya kukosa utulivu kwa macho yake. Anaona vitu ambavyo sioni, kama mchoraji anayeishi enzi za mashini.

Na kwa nini asiwe hivyo? Katika umri wa miaka 30, ametoka Geneva (Uswizi) ambako amekuwa akilea kikundi cha Wakenya katika roboti kwa Shindano la Kwanza la Kimataifa (Shindano la kila mwaka ambalo linalenga taaluma ya STEM - Sayansi, Tekinolojia, Uhandisi na Hisbati - masomo na ajira kwa vijana.)

"Ni kama mashindano ya Olimpiki, lakini ya roboti," anasema. "Au kama Kombe la Dunia kwa roboti," ninaongeza.

Hilo ni kando na kazi yake ya kila siku kama kiongozi wa kampuni ya VENO Autobotics, ambayo lengo lake ni kutoa Afrika katika kuwa mtumiaji teknolojia hadi kuwa mdau mkuu katika sekta hiyo. Autobotiki, kwa wasioelewa, ni kuunganisha mitambo inayoendeshwa na Roboti. Haziwezi kutenganishwa na ndugu yao, programu za kompyuta. Kama programu hizi ni damu katika sekta ya teknolojia, basi autobotiki ni moyo unaopiga damu.

"Katika autobotiki, kuna uhandisi wa programu na usio wa pogramu za kompyuta. Programu za kompyuta ndizo zimejulikana sana, huku Google na Amazon zikiajiri wengi wanaoziunda (nchini Kenya). Sehemu isiyo ya kompyuta ndiyo tunajaribu kushughulika nayo, IoT (Internet of Things) na sehemu yake inayohusu teknolojia zaidi, ambayo ni robotiki."

Namwambia ni sawa tu, jinsi ya kiwavi kufanya kazi yote lakini kipepeo anapata umaarufu. Anacheka "IoT ni uwezo au jinsi kazi inavyofanyika," ananieleza kama mtoto wa umri wa miaka mitano. Ni njia ya mawasiliano ya vifaa. Tatizo ni kuwa robotiki inahitaji pesa nyingi, lakini biashara yetu kuu hasa ni IoT. Tunazijenga kufuatilia biashara na kutokana na majukumu ya biashara husika"

VENO inajivunia kuunda mifumo ya teknolojia kwa Baridi, Quepay, Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru ya Kenya, Taasisi ya Utafiti Kuhusu Wanyama Wanaohusina na Binadamu, Serikali ya Kaunti ya Elgeyo Marakwet, Cheche Electronics na Medcure Healthcare.

Lakini haya yote yalianza wapi? "Nilipokuwa mdogo, nilipenda kujua jinsi ambavyo vitu vinafanya kazi, na nikawa nafungua DVD na redio. Nililelewa kijijini kwa hivyo nilichoweza kufanya ni kucheza na vitu. Nilipenda sana kuvitenganisha na kuviunganisha haraka."


Kijiji anachozungumzia ni Elgeyo Marakwet, lakini ukitaka maelezo zaidi, ni Kapsowar, kilomita 374 kutoka Nairobi. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi, ambako alihitimu digrii ya uhandisi wa mitambo ya stima na elektroniki.

Ni hapo ambapo alipata mshtuko, mchezo kando: hakukuwa na kazi halisi ya stima. "Ilikuwa nadharia zaidi kuliko kazi yenyewe. Iwapo ulitaka kazi yenyewe, kama nilivyotaka, ulipaswa kuanzia kiwango cha diploma."

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

**Roboti ya kweli hasa ni binadamu. Kwa binadamu, kuna sehemu ya umaizi wake. Hicho si kitu unachoweza kuunda katika programu, labda uandike kila sehemu. Kitu cha pekee kinachotuvutia katika roboti ni udhibiti, ambacho huwezi kupata katika binadamu.**

Victor Boit



Moja ya roboti zilizoundwa na Victor wa Boit wa Veno Autobotics. PICHA | JEFF ANGOTE

Ili kutimiza kitu cha maana maishani, lazima utie bidii. Boit ananifunza sanaa ya kutosubiri mambo kufanyika, kulenga mbali na kila wakati kudhibiti mkondo wako. Kwake, kufaulu ni kuhusu kulenga mbali na si vitu vya haraka. Ni maneno ya moja kwa moja ya hekima ya wazee wenye busara, yanayotamkwa haraka. Inaibuka kuwa unapojiamini mwenyewe, dunia haina chaguo isipokuwa kukubali nia yako.

Uchunguzi wa haraka kuhusu miradi ambayo amehusika nayo unafichua haya. VENO Autobotics imejenga mifumo ya maziwa, mifumo ya malipo na kwa wakati huu inajenga mfumo wa maegesho ambao unahusu kuweka sensa za kutambua hali katika majumba ya biashara na maegesho.

"Pia tunajenga IOT ya suluhu kwa usimamizi wa jiji la kisasa: kwa mfano, kama wanataka mita za kisasa za maji, wanaweza kuona ni sehemu gani zinatumia maji kwa wingi."

Mradi huu wa hivi punde, ananong'oneza, ni kwa ushirikiano na serikali fulani. Ninamdadisi kujua ni gani, lakini anakataa kabisa.

Baridi ilikuwa moja ya kampuni za mwanzo ambazo VENO Autobotics ilifanyia kazi. Baridi inajenga vyumba vya baridi kama njia ya kuongeza thamani nyama sokoni, kuzuia nyama kuharibika kwa kutumiwa kama stoo. Ni uhandisi wa kipekee unaotumia kawi ya jua na IoT inayojumuisha sensa za kiwango cha joto, sensa za milango na uwezo wa kukusanya data.

Anazungumzia mradi wa Baridi kwa majivuno ya bab mwenye mtoto aliyewekea matumaini makubwa anapotimiza na kuzidisha uwezo wake.

VENO ni ufupisho wa majina matatu, ya marafiki watatu: Victor (mwenyewe), Enoch na Nobert. Ni Victor aliyebaki. Kitu kimoja kuhusu biasharani ni kuwa ni mke mwenye wivu; inahitaji umakini wako wote.

"Watu hawatambui kuwa, mnapoamua kuingia katika kazi, mnafanya kazi saa 24/7. Hakuna kupumzika unapomiliki biashara. Lazima ulipe watu na kuridhisha wateja, ili biashara iendelee."

Kwa wakati huu, VENO ina wafanyakazi sita - wahandisi sita wa programu za kompyuta, mmoja anayeshughulikia maudhui na wawili wa uhandisi usio wa kompyuta ambao Victor mwenyewe anapenda huku akisimamia biashara kwa wakati mmoja.

Hillary Chesebe, mshauri wa kiufundi na mtaalamu wa kawi katika VENO, hana kingine isipokuwa upendo kwa Victor. "Ananipa motisha. Tulikutana Qatar akitoka kutoa mafunzo ya ulezi (Geneva), na akanipat nafasi ya kufanya kazi naye. Anawaamini vijana na anawapa majukumu. Anawapa watu nafasi na alinipa nafasi." Umewahi kumweleza hayo, nauliza.. "Hapana, lakini natumai atayasoma hapa. Kama ningemwelezea kwa neno moja, lingekuwa 'mwerevu'."

Kuhusu werevu, Victor anahisi anashindana na Mungu, au anajichukulia kuwa mungu mdogo? "Hata! Kwa hakika, kuna baadhi ya mambo ambayo hata sayansi yenyewe haiwezi kuelewa yalivyo. Kama akili ya binadamu, kitu cha ajabu."

"Roboti ya kweli hasa ni binadamu." Anasema haya kwa sababu ninamuuliza iwapo wanadamu ni kama roboti au iwapo roboti ni kama binadamu. "Kwa binadamu, kuna sehemu ya umaizi wake. Hicho si kitu unachoweza kuunda katika programu, labda uandike kila sehemu. Kitu cha pekee kinachotuvutia katika roboti ni udhibiti, ambacho huwezi kupata katika binadamu."

Anasikika kama mtu anayefikiria sana. "Naam, mimi nafikiria kwa mantiki sana."

Ni wakati gani ambao mantiki yake ilimfeli? "Kwa mambo ya uajiri, unapojaribu kupata mtu akufanyie kazi na unakosa kuzingatia vigezo vingine vinavyohusika. Hadi unapogundua hakuna sababu ya mtu kufanya kitu kingine ilhali wanakifanya."

Anaugama kuwa anapenda kusimamia kila kitu. Kwa mtu anayependa kusimamia kila kitu, wakati wa pekee anaoruhusu mambo yafanyike bila kuhusika kwake ni anapokuwa na watu anaowaamini karibu naye. Kuna mambo yanayomkosesha uzingizi usiku? "Ndio. Zaidi kufeli. Nikifanya kila niwezalo na ninakosa kufaulu. Hilo litanifadhaisha."

Kuna kitu anachojutia katika maisha yake? "Ndio. Kuna biashara nilizoanzisha na kuacha zilipofeli. Ningejua ningezifanya na kuendelea kuzifanya tena na tena, ningekuwa mbali sana. Hilo ndilo ninalojutia sana." Hilo na lile la kukosa kufungua TV.

***eddyashioya@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

## HATUA MUHIMU

**KRA** – Aliunda muongozo wa jinsi ya kujaza malipo ya ushuru. Ni muongozo wa hatua kwa hatua kuhusu stakabadhi zinazohitajika na jinsi ya kuzijaza.

**IPR(Institute of Primate Research Karen)** - Alijenga na kuweka mfumo wa kutumiwa na wafanyakazi kuingia na kutoka kazini na mwingine wa kuonyesha wakati ambao mtu anafaa kusemekana amechelewa ama amefanya kazi muda wa ziada.

**Serikali ya Kaunti ya Elgeyo Marakwet** – Alisambaza kompyuta kwa Sh1.4 milioni.

**Medcure Healthcare Ltd** - Alijenga mfumo wa kuwezesha malipo kupitia m-pesa.

**Cheche Electronics** – Aliwajengea tovuti ya kibiashara.

Nation Media Group "ePaper Copy"

UTIRIRISHAJI MUZIKI KIDIJITIALI

# MUZIKI MTAMU KWA MASIKIO YA WASANII

**UPAKUAJI:** Kando na kuwapa wapenzi wa muziki chaguo zaidi za kupakua muziki wa humu nchini na wa kimataifa, kupanuliwa kwa majukwaa ya utiririshaji kunamaanisha kuongezeka kwa mapato ya wanamuziki wa Afrika

● NA SINDA MATIKO

Tangu 2010, huduma za muziki dijitali zilipoanzishwa Afrika kupitia majukwaa ya utiririshaji sauti kama vile Simfy Africa ya Afrika Kusini, Iroking nchini Nigeria na Mdundo nchini Kenya, vituo vingine vimeibuka kote barani, na kuwapa wapenzi wa muziki njia ya kupata muziki wa humu nchini na wa kimataifa.

Mashirika makubwa duniani yameanza kufurika barani. Mnamo Aprili 2020, Apple Music, ambayo ilikuwa ikipatikana katika nchi 13 pekee za Afrika, ilipanua shughuli zake hadi mataifa 25 zaidi. Kisha mwaka mmoja uliopita, Spotify, iliyoanzishwa 2006 na inayoweza kutajwa kuwa jukwaa maarufu zaidi la utiririshaji sauti ulimwenguni, iliamua kuingia katika nchi 40 za Afrika ikiwemo Kenya.

"Tulichukua muda katika upanuzi huo ili kuhakikisha tulifahamu jinsi ya kuungana na wapenzi wa muziki wa Kenya na watengenezaji. Kila soko ni tofauti kwa hivyo, kuelewa vyema ni muhimu," Phiona Okumu, Mkuu wa Muziki wa Spotify katika mataifa yaliyo chini ya Sahara, akaambia safu ya Vijana.

Zaidi ya kuwapa wapenzi wa muziki chaguo zaidi, kupanuliwa kwa majukwaa ya utiririshaji sauti pia kunamaanisha kuongezeka kwa mapato ya wanamuziki wa Afrika.

Lakini hatua hiyo imejiri na changamoto, ikiwemo gharama ya juu ya data ya simu za mkono.



Kenyan musician Vivian Wambui.

Ripoti moja ya wataalamu wa data za masoko na watumiaji, Statista, inasema mataifa ya chini ya Sahara yanaongoza kwa bei za juu zaidi za data ulimwenguni, huku Equatorial Guinea ikiongoza.

Afrika Mashariki ina bei za chini za data barani Afrika: Tanzania inaongoza kwa dola za Amerika 0.17 (Sh20) kwa 1 GB, kwa mujibu wa Cable.co.uk, na Kenya inafuatia ikiwa na bei ya dola za Amerika 0.84 (Sh100) kwa I GB. Hii inaeleza sababu ya kampuni nyingi za utiririshaji sauti kulenga nchi hizi mbili za Afrika Mashariki.

"Kanda hii ina watu 537 milioni, wengi wakiwa na umri wa miaka 35 na chini. Jijini Nairobi, asilimia 80 ya watu wana simu za kisasa. Hawa ni watu wanaopenda muziki," anasema Cleopatra Mukula, Mkuu wa Biashara ya Muziki Mashariki na nchi zinazozungumza Kiingereza Afrika katika kampuni ya Trace TV.

Hivi ndivyo vigezo ambavyo vilivutia Spotify na Apple Music katika soko la Afrika Mashariki huku TIDAL, iliyoanzishwa na mwanarapa bilionea wa Amerika, Jay Z, ikiingia soko la Afrika Kusini na Uganda mnamo 2018. Mwaka jana, TIDAL ilianzisha kituo cha African Music Hub.

Jambo la kutamausha ni kuwa ni wasanii wachache wa Kenya ambao wamejisajili katika majukwaa haya ya kimataifa yanayolipa vizuri. "Hii inavunja moyo kwa sababu Spotify na Apple Music zinalipa vizuri na sasa ziko hapa," akasema Camila Owora, anayefanya kazi na kampuni ya kusambaza muziki ya Zikki Music.

"Wasanii wetu wanajivuta kuingia katika majukwaa haya

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Phiona Okumu, Msimamizi wa Muziki wa kampuni ya Spotify eneo la Afrika chini mwa Sahara.

kwa sababu huduma hizo zilianzishwa majuzi katika eneo hili na wengi hawajui jinsi ya kufanya hivyo. "Wasambazaji wa Muziki wanaweza kuwa daraja la kuwaingiza katika tovuti hizo na kuwasaidia kupata faida ya muziki wao," akaongeza Owora.

Tangu Januari 2021, kumekuwa na ongezeko la asilimia 25 ya idadi ya wasanii wa Kenya katika Spotify. "Zaidi ya nyimbo 8,000 zimeongezwa katika tovuti hiyo tangu ilipozinduliwa rasmi Kenya. Nafikiri ni vyema kusema kuwa mwelekeo wa ukuaji wetu una matumaini," akasema Okumu.

Mnamo Aprili 2022, Spotify ililipa dola za Amerika 7 bilioni kwa wamiliki rasmi wa haki za muziki ikiwa ni dola 2 bilioni zaidi ya ilizolipa 2020 na zaidi ya maradufu ya ilizolipa 2017.

Wakati huo huo, kampuni ya Boomplay ilianzishwa Agosti 2015 nchini Nigeria na Mdundo ikaanzishwa Kenya mnamo 2012. Kampuni hizo mbili zilizua ushindani katika soko la kikanda, kwa ukuaji mzuri katika miaka michache iliyopita. Ikiwa na watumiaji 60 milioni, kampuni ya Boomplay, inayomilikiwa na China, ndiyo maarufu zaidi ya utiririshaji wa muziki Afrika.

"Boomplay ni jukwaa linalokua. Mapato si ya juu lakini yanaongeza thamani kwa kusaidia wasanii na uuzaji," anasema mwimbaji wa Chum Chum, Vivian Wambui.

Boomplay inadai ina muundo mzuri wa mapato Afrika. "Kampuni hiyo inafadhiliwa na wawekezaji na pia inapata pesa kupitia matangazo, ambayo yanagawanywa kati ya msanii na Boomplay. Wasanii wanaweza kujadiliana mgao wa asilimia 70 - 30 au asilimia 60 - 40, asilimia ya juu ikimwendea msanii," duru ya ngazi ya juu ikafichulia jukwaa la Vijana. Boomplay pia hulipa mrahaba kwa kutegemea jinsi muziki wa mtu unachezwa kwa wingi. Malipo hufanywa mara nne kwa mwaka, lakini ni lazima atimize kiwango kinachowekwa. "Usipotimiza kiwango hicho basi kinasongeshwa mbele," zikaongeza duru zetu.

Muundo wa Boomplay ni tofauti na ule wa Mdundo, ambayo juzi ilitangaza kuwa italipa Sh100 milioni mwaka huu wa kifedha kwa wamiliki wa haki za muziki, kiwango cha juu zaidi tangu ilipoanzishwa.

Ikiwa na watumiaji 20.3 milioni kote Afrika kufikia Juni 2022, milioni 4.6 kutoka Kenya, chanzo kikuu cha mapato cha Mdundo ni matangazo ya biashara kupitia mabango na sauti katika video za muziki wake. Pia, imeorodheshwa katika soko la hisa la Denmark kusaidia kuharakisha ukuaji wake katika mataifa ya chini ya Sahara.

Martin Nielsen, mwanzilishi mwenza na Afisa Mkuu Mtendaji, anahusisha ukuaji wa Mdundo na uwezo wake wa kufikia soko kubwa. Ina muundo wa kipekee wa kifedha unaozingatia msanii: Wasaniii 100,000, kati yao 20,000 wakiwa Wakenya ambao wamejiunga na jukwaa hilo, waligawana na Mdundo nusu kwa nusu mapato yote yaliyotoka kwa mrahaba. Wakati wa malipo, mgao wa kupakuliwa kwa kazi ya msanii unahesabiwa na kuongezewa jumla ya mrahaba kubaini anachopaswa kupata.

"Tunaangalia kiwango ambacho muziki unatumiwa. Cha msingi ni kuwa tunalipa kulingana na upakuaji na wasanii wanaweza kufuatilia idadi ya upakuaji na mapato yao. Inategemea idadi," anaeleza Nielsen.

Muziki wa Injili ndio unatumiwa sana katika Mdundo nchini Kenya na kote katika soko la Afrika, ukiwa asilimia 11, ukifuatwa na muziki kutoka Nigeria, maarufu kama Naija kwa asilimia 9.

Msanii wa nyimbo za injili David Wonder anakubaliana naye. "Walinilipa Sh4,000 kwa upakuaji mara 14,000. Lakini Boomplay bado wako mbele. Katika muda huo, muziki wangu ulikuwa umepakuliwa zaidi ya mara 800,000 katika Boomplay. Boomplay inamtangaza msanii sana, jambo ambalo nafiriki Mdundo inafanya pia."

Mwanamuziki wa Ohangla, Prince Indah, anafanya vyema katika Mdundo na Boomplay. "Nafurahishwa na Boomplay. Mdundo inafaa kuiga baadhi ya mawazo yao."

Nielsen anakubaliana na maoni haya lakini anaongeza kuwa kwa wakati huu, wanapojitahidi kuimarisha jukwaa hilo, kitu muhimu kufanya ni msanii kuwa katika jukwaa hilo kwa sababu kuna kitu cha kupeleka nyumbani badala ya muziki wao kupakuliwa bila malipo kutoka kwa tovuti ambako unawekwa na walanguzi kinyume cha sheria.

***tmatiko@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*







ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

tahariri




■ Rais anahofia maandamano barabarani dhini ya serikali yake

# Ruto anamhitaji Kalonzo upande wake



KWENDO
OPANGA

Rais William Ruto na Naibu wake Rigathi Gachagua wanasema wamemuomba Kalonzo Musyoka ungane nao serikalini. Lakini, anasema Rais, Musyoka, ambaye amewahi kuwa makamu rais, amekataa pendekezo hilo kwa sababu anataka kuwa katika upinzani. Naibu Rais, kwa upande wake, anasema hawamuelewi mwanasiasa huyu mwenye ushawishi katika eneo la Ukambani.

Hata hivyo, Seneta wa Makueni, Daniel Maanzo, ambaye ni mshirika wa Musyoka, anasema Rais na Naibu wake wanataka Musyoka awaunge mkono ili wabunge wa Wiper warudi upande wao ili wapate asilimia 65 ya wabunge wanaohitaji kubadilisha katiba.

Hali tano tofauti zinajitokeza kuhusu mikakati ya Rais Ruto ya baada ya uchaguzi mkuu. Moja, yeye na naibu wake bado hawajatulia katika nyadhifa zao, licha ya kuvutia idadi kubwa ya wabunge iliyowawezesha kuwaweka wapinzani wao wa Azimio upande wa walio wachache na kunyakua wadhifa wa Spika wa Bunge la Kitaifa kutoka kwao.

Baada ya kitimiza hilo, sasa wajibu wa kulalamika na kuhakikisha serikali inawajibika umo mikononi mwa walio wachache katika Bunge na wanachama wao. Wajibu wa Rais na Naibu wake ni kutawala na kutekeleza ahadi walizotoa kwa raia.

**Rais aliendesha kampeni ya kupinga mabadiliko ya katiba ili kubuni nyadhifa kwa wanasiasa washirika wa vigogo wakuu. Badala yake alipendekeza juhudi zielekezwe katika kukuza uchumi ili kuzalisha nafasi za ajira kwa wote. Lakini sasa anataka kutumia njia za mkato kulinda maslahi yake.**

Pili, mnamo 2016, Rais alimcheka Musyoka aliporushiwa vitoa machozi na kupigwa picha akiketi kwenye lami aliposhirikiana na Bw Raila Odinga kuongoza maandamano dhidi ya serikali.

Lakini licha ya kushikilia mamlaka, Rais bado anahofia maandamano dhidi ya serikali yake. Maandamano yalichangia maridhiano kati ya Odinga na Rais Kenyatta, yaliyomtoa katika serikali. Na, kama Rais anavyoelezea, hali hiyo ilimlazimu kupinga serikali ambayo alibuni pamoja na rais mstaafu Kenyatta.

Rais Ruto ana wasiwasi kwa sababu wananchi wanalalamika kuhusu kupanda kwa bei za vyakula, licha ya ahadi yake ya kupunguza gharama ya maisha.

Tatu, Musyoka atagombea urais dhidi ya Rais katika uchaguzi mkuu wa 2027 na akiungwa mkono na Odinga, atakuwa mpinzani mkali. Rais Ruto anaogopa kwamba wawili hao wakiamua kuongoza maandamano dhidi ya serikali yake, hali hiyo itakuwa pigo kubwa kwake. Hatua hiyo ikiungwa mkono na wabunge, itavuruga ajenda ya serikali yake.

Rais Ruto hajamaliza kazi Ukambani na ndiyo sababu namfuata Musyoka. Anataka amuunge mkono ili aweze kudhibiti eneo hilo kisiasa. Lakini Musyoka analenga 2017 kama nafasi yake nzuri ya kuwa rais na amejipatia sura ya rais mtarajiwa.

Nne, Rais Ruto ameonyesha dalili kwa Odinga kwamba yuko tayari kwa maridhiano naye.

Lakini Odinga na washirika wake, hasa katika Kaunti ya Homa Bay, ambako Ruto alizuru juzi, walijitenga na ziara hiyo.

Haya yanajiri wakati ambao Musyoka anajipanga kuwa mrithi wa kura za ngome ya Odinga, kwa misingi kwamba amemuunga mkono mwanasiasa huyo mkongwe tangu 2013.

Rais anadhani ni rahisi kumvuta Musyoka kutoka kwa Odinga badala ya kumkuza kigogo mwingine wa kisiasa kuchukua nafasi ya Odinga katika eneo la Luo Nyanza.

Mwisho, Rais aliendesha kampeni ya kupinga mabadiliko ya katiba ili kubuni nyadhifa kwa wanasiasa washirika wa vigogo wakuu. Badala yake alipendekeza juhudi zielekezwe katika kukuza uchumi ili kuzalisha nafasi za ajira kwa wote. Lakini sasa anataka kutumia njia za mkato kulinda maslahi yake. Je, Musyoka ataweza kumzima? Amekuwa akiahidi kuunda Baraza la Mawaziri la pembeni, na hiyo ni sawa. Lakini bado hajatimiza ahadi hiyo.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

■ Katika nyika za Samburu na Laikipia, huenda kuna mrithi mwingine wa ufalme Uingereza

# Operesheni CBE: Mtu wetu atawala Himaya



MACHARIA **GAITHO**

Iwapo bado anadumisha mtindo wake wa kuzingatia wakati, ni lazima Rais Wiliam Ruto afanye haraka na kupandisha bendera ya Kenya nchini Uingereza.

Kuchaguliwa kwa mtu wetu, Rishi Sunak, kuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, ni hatua ya mwisho ya safari ndefu ya kugeuza hali katika taifa hilo la waliokuwa watawala wetu kutoka kwa changamoto za kiuchumi na misukosuko ya kisiasa.

Kwa miongo michache iliyopita, ushawishi wa taifa hilo, ambalo lilikuwa miongoni mwa nchi zenye nguvu zaidi duniani, umepungua sana. Kujitenga kwake na hali ya kutekwa na watu wenye chuki na ubaguzi, kumeligeuza kuwa taifa pweke ambalo usemi wake hauwezi kusikika Ulaya, wala mataifa iliyotawala.

Huu ndio wakati mwafaka wa kumaliza Operesheni CBE (Ushindi Dhidi ya Himaya ya Uingereza). Rishi Sunak kuchaguliwa Waziri Mkuu wa Uingereza si ajali, bali mchakato ambao umekuwepo kwa muda mrefu.

Kwa namna moja, kupanda kwake kunaweza kufananishwa na safari ya aliyekuwa rais wa Amerika, Barack Obama, ambaye baba yake alikuwa miongoni mwa mamia ya Wakenya wachanga walioenda Amerika miaka ya 1950 kusoma. Wakiwa huko, walipata watoto ambao baadaye walichukua uongozi wa taifa lenye nguvu zaidi duniani.

Mpango huo ulianza baba ya Rishi, Yashvir Sunak na maelfu ya washirika wake kutoka Kenya wenye asili ya Afrika Kusini, waliposhawishiwa kuhama mitaa iliyokuwa mitaa ya kifahari ya South C, Nairobi West, Ngara na Parklands, kuelekea miji ya London, Birmingham, Southampton, Liverpool, Manchester, kati ya miji mingine mikubwa nchini Uingereza

Walikuwa kama 'wageni' waliojiongeza katika jamii ya Waingereza; waliokuza biashara zao ndogo hadi wakapata ushawishi katika sekta ya biashara na viwanda, na hatimaye kujitosa katika siasa.

Haikuwa sadfa, kwa mfano, kuwa hatua ya Suella Braverman kujiuzulu kama Waziri wa Mambo ya Ndani, ilichangia kuanguka kwa aliyekuwa waziri mkuu wa taifa hilo Liz Truss. Braverman anatoka jamii ya Wagoa, ingawa ana asili ya Kenya na Afrika Kusini.

Mapema mwaka huu, baba yake, Christie Fernandes, aliambia gazeti la Times of India kuhusu mazungumzo waliyowahi kuwa nayo familia yake wakiwa likizoni nchini Amerika: "Nilimwambia kama Obama alifanikiwa nchini Amerika licha ya kutoka Kenya, anaweza pia kufanikiwa nchini Uingereza."

Baadaye, Suella alifanikiwa kushikilia moja ya nyadhifa za uwaziri zenye ushawishi mkubwa sana, inayolingana na Wizara ya Usalama wa Ndani hapa Kenya.

Operesheni CBE haiwahusu Wahindi wenye asili ya Kenya tu. Kote nchini Uingereza, kuna maelfu ya Wakenya wenzetu waliochukua uraia wa taifa hilo ambao wanahudumu katika taaluma tofauti, mabaraza ya miji, uchukuzi, afya, elimu, usalama na majukumu mengine katika sekta za kibinafsi na umma. Wengi wetu tuna marafiki na jamaa ambao wanangoja tu kupuliziwa kipenga.

Kando na jamaa zetu walio huko, naweza kudai uhusiano baina yangu na Suella, unaotokana na Shule ya Ribero Goan (Parklands), alikosomea baba yake. Pia, ndiyo shule nilikosomea mimi na ndugu zangu wengi.

Inaweza kufichuliwa kuwa Opereshenі hiyo ambayo ndiyo imechangia Mtu wetu kuchukua uongozi nchini Uingereza, haikuanza na kuhamishwa kwa Wahindi wenye asili ya Kenya katika miaka ya 1960 na 1970.

Johnstone Kamau wa Ngengi au Jomo Kenyatta alipotumwa jijini London na chama cha Kikuyu Central Association (KCA) mnamo 1929, jukumu lake halikuwa tu kupiga vita ukoloni wa Uingereza nchini Kenya, bali pia 'kupanda mbegu' kama Obama na wengine waliokuja baada yake.

Matokeo yake yalikuwa kuzaliwa kwa Peter Magana, kutokana na ndoa baina yake na mwanamke Mwingereza, Edna Clarke. Magana alizaliwa mnamo 1944 eneo la Sussex Magharibi. Mama yake alibaki nchini Uingereza Kenyatta aliporudi Kenya 1946 kuongoza harakati za kupigania uhuru, uliopatikana baadaye 1963. Magana hakujitosa katika siasa, bali alihudumu katika uanahabari. Alipiga hatua hadi kuwa produsa wa cheo cha juu katika Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC). Sasa amestaafu.

**Kando na jamaa zetu walio huko, ninaweza kudai uhusiano baina yangu na Suella, unaotokana na Shule ya Ribero Goan (Parklands), alikosomea baba yake. Pia, ndiyo shule nilikosomea mimi na ndugu zangu wengi. Inaweza kufichuliwa kuwa Operesheni hiyo ambayo ndiyo imechangia Mtu wetu kuchukua uongozi nchini Uingereza, haikuanza na kuhamishwa kwa Wahindi wenye asili ya Kenya katika miaka ya 1960 na 1970.**

Majengo aliyoishi Kenyatta jijini London, 95 Cambridge Street, Pimlico, London SWIV 4PY na City of Westminster, yamewekwa picha zake na Taasisi ya Kusimamia Turathi za Uingereza. Taasisi hiyo ndiyo hulinda na kusimamia maeneo ya kihistoria, majengo na sehemu zingine.

Huku mtu wetu akiwa uongozini, kwa sasa tunaweza kutarajia kuongezwa kwa ufadhili wa juhudi za kuhifadhi maeneo yanayosimamiwa na taasisi hiyo. Zaidi ya hayo, tunafahamu Waziri Mkuu huyo atakuwa akiripoti kwa Rais Ruto, anayetarajiwa kuwa miongoni mwa viongozi wa kwanza kualikwa kwa ziara rasmi ya kiserikali nchini Uingereza, baada ya Mfalme Charles III kutawazwa rasmi.

Hadithi kuhusu jinsi mama ya Charles, marehemu Malkia Elizabeth II alivyochukua uongozi wa kifalme akiwa ziarani Kenya inajulikana vizuri. Yasiyojulikana sana ni kuwa, akiwa kijana mdogo, Mwanamfalme Charles alifanya ziara kadhaa nchini Kenya. Kuna wanaojua kuhusu watoto wake aliowapata akiwa humu nchini, ambapo kadri wakati utakavyosonga, wataidhinishwa kuwa wa kwanza kwenye orodha ya watakaomridhi.

Kwa sasa, wa kwanza katika orodha hiyo ni Mwanamfalme William, ambaye pia anapenda Kenya, hilo likidhihirika alipokuwa akimchumbia mkewe, Kate Middleton.

Mahali fulani katika nyika za Samburu na Laikipia, huenda kuna mrithi mwingine wa ufalme Uingereza mwenye asili ya Kenya.

Huwa tunasema historia hujirudia. Katika mahusiano yetu na nchi iliyotutawala, hali imegeuka kuwa kinyume. Uwaziri Mkuu ni mwanzo tu. Kitakachofuata ni Ufalme. Hebu fikiria, wawekezaji wa kibinafsi Kenya watafanyia nini majengo yote mazuri na yasiyotumika jijini London na kwingineko nchini Uingereza, Scotland na Wales? Na maeneo yote katika kisiwa cha Jersey ambako watu matajiri huficha pesa zao yatakuwa yetu pia! Uingereza, twaja!

***gaithomail@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

WAUME WA MAGAVANA

# MAJUKUMU YAKIENDA KINYUME

*Mume wa gavana akihusika katika masuala ya mkewe atalaumiwa kwa kuingilia mambo yasiyomhusu. Lakini kanuni hiyo haitumiwi kwa wake wa magavana, ambao wanahusika sana katika shughuli za waume wao*



**Kamotho Waiganjo akigawana kipande cha nyama na mke wake, Anne Waiguru, wakati wa harusi yao ya kitamaduni katika Shule ya Msingi ya Kiamugumo, Kaunti ya Kirinyaga, mnamo Julai 13, 2019.** PICHA | JOSEPH KANYI

• NA OSCAR OBONYO

Wanaume hawafurahii kuonekana kushikilia nafasi za chini ya wake zao mbele ya umma, hasa katika jamii yetu ambayo inaweka wanaume juu. Utata unaibuka zaidi katika hali ambapo wanaume ndio wachache miongoni mwa kundi la wake magavana, ilivyo sasa nchini Kenya.

Murega Baicu, mumewe Gavana wa Meru, Kawira Mwangaza, ambaye katika siku za hivi karibuni ameangaziwa na vyombo vya habari akisimama kando ya mkewe, anasema ni mwathiriwa wa "dhuluma za kijinsia."

Mume wa Gavana wa Meru haelewi ni kwa nini watu hawataki kumuona kando ya mkewe ofisini mwake, katika shughuli za umma au hata katika gari lake rasmi ilhali hawakulalamika magavana wa zamani Peter Munya na Kiraitu Murungi walipoandamana na wake zao katika shughuli za umma.

"Hali hii inanikanganya. Ninaiga tu kile ambacho Bi Munya na Bi Kiraitu wamekuwa wakifanya lakini watu – hasa Madiwani hawataki kuniona karibu na gavana. Nadhani watu wangu wa Meru hawajazoea hali ya mwanamume kuwa "Mke wa Gavana"," anasema, akicheka.

Murega hasa amelaumiwa kwa madai ya kuwapa maagizo Madiwani, kuwakaripia wafanyakazi wa kaunti na kutekeleza wajibu wa mfichuzi wa sakata, hatua anayodai inalenga kuzuia wizi wa fedha za umma. Gavana ameemteua kuwa Mlezi wa Shirika la Huduma ya Vijana Meru na pia "balozi wa Mahasla wa Meru".

Mwenzake wa Kirinyaga, Kamotho Waiganjo, mumewe Gavana Anne Waiguru, anakumbuka hali tata aliyojipata wakati wa muhula wa kwanza wa mkewe.

Wakati mmoja nusra azuiwe kuingia katika hafla ya wenza wa magava kwa sababu waliandaa hafla hiyo walitarajia wanawake pekee.

Hatimaye aliruhusiwa kuingia baada ya kuelezea wapokezi wageni - ambao walikuwa wameagizwa wasiruhusu wanaume katika ukumbi wa hafla hiyo - kwamba alikuwa mwathiriwa wa dhana ya waandalizi kuwa magavana wote huwa wanaume.

Kufuatia tukio hilo la aibu, Waiganjo ananuia kupendekeza jina la Muungano wa Wake wa Magavana (CFLA) libadilishwe ili kushirikisha jinsia zote mbili. Kama sivyo, waume wa magavana wanaweza kubuni muungano wao.

Waiganjo anasema hali hiyo ya kukanganya, na kutoelewa kuhusu nafasi yake inatokana na imani ya jamii inayomtukuza mwanamume. "Wajibu wetu hapa ni kubaini ukweli kuwa hakuna mipaka ya kijinsia katika masuala ya utawala. Tunafaa kukipa cheo cha ugavana maana inayoeleweka na wote; ili watu wengine wasituone kuwa viumbe wa kiajabu." anasema.

Lakini kulingana na jamii yetu, mwanamume akijihusisha na shughuli za mkewe, atalaumiwa kwa kuingilia mambo yasiyomhusu. Lakini kanuni hiyo haitumiwi

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



Gavana wa Homa Bay Gladys Wanga na mumewe George Wanga. PICHA I MAKTABA



Gavana wa Nakuru Susan Kihika na mumewe Sam Mburu.
PICHA I CHEBOITE KIGEN



Gavana wa Kwale, Fatuma Achani na mumewe, Ali Kanga. PICHA I SIAGO CECE



Gavana wa Meru, Kawira Mwangaza na mumewe, Murega Baicu. PICHA I DAVID MUCHUI

kwa wake wa magavana ambao mara nyingi wanashiriki sana mipango na shughuli za waume wao.

Waiganjo na Murega wanasema kuwa hali hiyo hukubalika kwa sababu huchukuliwa kuwa ya kumsaidia gavana.

Labda hiyo ndiyo sababu Murega analaumiwa na baadhi ya raia katika Kaunti ya Meru kwa kuandamana na mkewe wakati wote, ofisini na katika mikutano rasmi, na ndiyo sababu, kwa upande mwingine, Waiganjo na Ali Kanga (mume wa Gavana wa Kwale Fatuma Achani) wameamua kutoonekana hadharani na wake zao.

Waiganjo ameamua, kimakusudi, kukaa kando ili mkewe "ahisi mkamilifu" na aonyeshe watu wa Kirinyaga kuwa anaweza kuendesha masuala ya kaunti hiyo "bila mwanaume kuonekana kando yake kila mara."

Badala yake, Waiganjo, ambaye ni wakili, humsaidia gavana kwa huduma za kisheria na ushauri kuhusu masuala ya uongozi na mikakati ya kisiasa. Lakini wajibu wake huo si rasmi.

Kanga pia hataki wajibu wowote katika serikali ya Kaunti ya Kwale. Anashughulika na kazi yake ya uhadhiri. Anaonelea ni bora akae kando na mkewe ili isidhaniwe kuwa anajaribu "kuingilia na kudhibiti shughuli za serikali hiyo." Kanga ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kiufundi cha Mombasa.

Hata hivyo, nafasi yake ipo kama Mume wa Gavana. Yeye ndiye kiongozi wa familia yake na kiungo muhimu katika shughuli za kisiasa na kimaendeleo zinazoendeshwa na mkewe.

"Wakati wa uchaguzi, ni lazima nitekeleze jukumu kuu la kuwaendea wanaume wenzangu kuwaomba kura zao. Jamii pia inatarajia kuwa nitasimamia usalama wake na kukinga familia yangu dhidi ya uvamizi wa kila aina – wa maneno au mwingine – wakati wa kampeni. Kwa hivyo, kimsingi, mke wangu, gavana wangu, ni wajibu wangu," ansema Kanga.

Lakini George Wanga, mumewe Gladys, Gavana wa Homa Bay, hataki kuonekana kando ya mkewe kila mara. Pia hataki kusema lolote kuhusu wajibu ambao atatekeleza katika serikali ya Homa Bay.

"Kuna sehemu yoyote ya Katiba inayozungumzia Wake wa Magavana au Waume wa Magavana?" akauliza Wamga na kukataa kuzungumza zaidi kuhusu nafasi hizo na majukumu ambayo hayajaelezwa katika katiba.

Vivyo hivyo, Dennis Apaa na Sam Mburu, waume wa Gavana wa Embu Cecily Mbarire na mwenzake wa Nakuru Susan Kihika, mtawalia, wanapendelea kukaa kando.

Wawili hao ambao ni wafanyabiashara, walikataa kabisa kuzungumza na "Darubini ya Wiki" kuhusu majukumu yao katika maisha ya kisiasa ya wake zao.

Kati ya kaunti saba zinazoongozwa na magavana wa kike, Machakos haina Mume wa Gavana.

Mume wa Wavinya Ndeti, Dolamu Henry Oduwole, raia wa Nigeria, alikufa Septemba 2016.

Majukumu rasmi ya Wake wa Magavana- na sasa Waume wa Magavana - hayaeleweki wazi-wazi. Wanaoshikilia nafasi hizi huwa na majukumu yasiyo rasmi na yasiyo na mshahara, kama vile kuhudhuria sherehe na shughuli rasmi, wakiandamana na gavana ama kwa niaba ya Gavana, na kusaidia katika mambo mbalimbali katika kaunti zao.

Mkanganyiko kuhusu nafasi hii pia unajitokeza katika ngazi ya kitaifa, hasa katika nchi ambako rais ni mwanamke. Katika taifa jirani la Tanzania, kwa mfano, Bw Hifidh Ameir, msomi wa masuala ya kilimo, anaishi kimya chini ya mkewe, Rais Samia Suluhu Hassan, aliyechukua uongozi wan chi hiyo mnamo 2021 kufuatia kifo cha mtangulizi wake, John Pombe Magufuli.

Kinyume na Waume wa Marais kote ulimwenguni, Bw Ameir, huwa haandamani na mkewe katika ziara za mataifa ya kigeni.

Jaji Mkuu mstaafu wa Malawi Richard Banda, hakuonekana hadharani mkewe, Joyce Banda, alipokuwa rais kati ya 2012 na 2014. Joyce, alimsifia mumewe kama "rafiki bora na kiongozi wa kushangilia) ambaye hakujiingiza katika shughuli zake za kisiasa.

Dhana potovu kuhusu wanaoshikilia vyeo vya Waume wa Magavana, inatokana na imani kuwa Wake wa Magavana ni 'mapambo' wasio na wajibu muhimu, na inawatatiza Waume wa Magavana.

Ili kuondoa dhana kuwa wao ni 'mapambo', Wake wa Magavana, chini ya mwavuli wa CFLA, wameanzisha mpango wa kimkakati wenye malengo mahsusi ya kutekeleza mipango ya kijamii, kiuchumi na kimaendeleo.

Mpango huo una mihimili minne ambayo ni kuvumisha, kuwezesha, kutoa huduma na kushirikisha. Ulizinduliwa na aliyekuwa Mama wa Taifa, Margaret Kenyatta, mnamo Julai 2015.

Lakini huku usawa wa kijinsia katika siasa ukiendelea kuimarika, kutokana na wanawake zaidi kushinda viti vya uongozi, idadi ya Waume wa Magavana inatarajiwa kupanda.

Uhalisia huu unaibua haja ya kuunda upya chama cha wenza wa magavana, ikiwemo kubadilisha jina, malengo na mipango ili kujumuisha jinsia zote.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "ePaper Copy"

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## Teknolojia ya LED yakuza miti

Akizungukwa na miche mingi ya miti iliyokuzwa kwa teknolojia ya LED, mtafiti wa masuala ya misitu, Kenny Hay, kutoka Scotland, amsema teknolojia hiyo inaweza kusaidia sana Uingereza kupunguza gesi hatari angani.

Miche hiyo iliyopangwa urefu wa mita tisa (futi 30) katika Taasisi ya James Hutton, Dundee, mashariki mwa Scotland, ni ishara tosha kwa Hay na wengine kuwa teknolojia ya LED inaweza kutumiwa kuharakisha ukuaji wake.

Kulingana na Idara ya Kusimamia Ardhi na Misitu ya Scotland (FLS), miti hiyo ilikua haraka mara sita zaidi, ikilinganishwa na muda ambao ingechukua kama ingekuzwa kwa njia ya kawaida.

Huenda majaribio hayo yakaleta mabadiliko mapya katika sekta ya misitu Uingereza na kusaidia serikali kutimiza malengo yake kupunguza gesi hatari angani.

Mpango huo unaendeshwa kwa ushirikiano na wataalamu wa kilimo wa shirika la Intelligent Growth Solutions (IGS). "Matokeo ya kwanza yalikuwa ya kutisha," akasema Hay, meneja katika FLS, akihojiwa na AFP wakati wa ziara maalumu katika shamba hilo.

"Tunaweza kukuza idadi kubwa ya miti katika eneo dogo sana, hali itakayotusaidia sana kudhibiti athari za mabadiliko ya hali ya hewa." "Tutaangalia jinsi tutajumuisha haya kwenye shughuli zetu za kawaida."

Kulingana na Hay, mradi huo "una uwezo mkubwa" wa kuzalisha miti. Majaribio hayo yalibaini kuwa miche hiyo ilikua kwa kati ya sentimita 40 na 50 (inchi 16-20) katika muda wa siku 90.

Kiwango hicho cha ukuaji kingechukua hadi miezi 18 katika hali na mazingira ya kawaida. Hewa iliyo katika shamba hilo ina unyevu na kiwango cha joto kinachohitajika kwa ukuaji wa miche hiyo.

Kulingana na Dave Scott, mwanzilishi wa shirika la IGS, watafiti wanaweza kubuni kiwango cha mwangaza, unyevu, maji, joto na aina ya mchanga kila mche unaohitaji. Kiwango cha maji na madini hudhibitiwa na hunyunyiziwa mimea kupitia mifereji kadhaa.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# GARI LA KUPAA ANGANI LINALOJIGEUZA NDEGE



**Mfano wa gari la kupaa angani inayojumuisha gari la kujiendesha na droni inayoweza kubeba mtu, kutoka kwa kampuni za Audi, Italdesign na Airbus. Kampuni ya Amerika inasema gari lake la kutumia umeme litaweza kupaa angani na kusafiri umbali wa kilomita 110.**

CALIFORNIA

Kwenye hafla ya uzinduzi katika Chuo Kikuu cha Draper, San Mateo, California, kampuni moja ndogo ilieleza jinsi gari lake linalopaa angani lilivyopangiwa kusafiri.

Kampuni ya Alef inataja gari hilo, linaloitwa Model A, na linaloendelea kutengenezwa, kuwa la kwanza litakalopaa angani kwa kweli.

Muundo wake unatarajiwa kuwa sawa na wa magari yanayotumia umeme, ingawa litakuwa na uwezo wa kupaa angani na kusafiri kilomita 110.

Kampuni hiyo inatarajia kubuni ushindani na mashirika mengine kama AirCar na Pal-V ambayo yamekuwa yakitengeneza magari kama hayo.

Lakini kulingana na Afisa Mkuu Mtendaji wa Alef, Jim Dukhovny, ambaye pia ni mmoja wa waanzilishi wake, magari mengi yaliyopo huwa hayapai angani kwa kweli. "Lazima gari linalopaa liwe la kweli. Hiyo inamaanisha kuwa linaweza kusafiri katika barabara ya kawaida na kuegeshwa katika maegesho ya kawaida. Pia, linapaswa kuwa na uwezo wa kupaa angani kutoka ardhini," akasema. "Kama utahitaji uwanja wa ndege ili kupaa angani, ni tatizo gani unalosuluhisha? Na, je, mbona hilo liwe gari linalopaa angani?"

Hata hivyo, kupaa kwa mwendo wowote bila usaidizi wa mabawa kutahitaji gari hilo kutumia kiwango kikubwa cha umeme.

Suluhisho linalopendekezwa na Alef ni jipya. Ili kusafiri kwa muda mrefu, gari hilo linajigeuza kuwa ndege yenye mabawa mawili, moja likiwa juu ya lingine.

Baada ya kuondoka ardhini, eneo la dereva pia linajigeuza ili kumwezesha kuliendesha vizuri.

Alef pia imetoa video inayoonyesha jinsi gari hilo linavyojigeuza Jarida la Forbes lilieleza kuwa gari hilo linajigeuza kama ndege aina ya Opener Blackfly, ambayo pia hutumia umeme. Ingawa ni uvumbuzi wa kipekee, swali ni iwapo unaweza kutekelezwa.

Inasemekana kuwa, kuunganisha masuala hayo mawili - kuliendesha na kupaa angani - kutahitaji kiwango kikubwa cha umeme.

"Muundo wake uko sawa kulingana na mahitaji ya kisasa ya kiteknolojia," anasema Profesa Steve Wright kutoka Chuo Kikuu cha West England, ambaye ni mhandisi wa vyombo vya kupaa angani.

Licha ya hayo, anasema huenda gari hilo likakumbwa na changamoto kujigeuza kwa muundo wa ndege baada ya kupaa angani.

Hata hivyo, Alef inasema imekuwa ikifanya majaribio kuhusu suala hilo tangu 2018 kupitia "safari kadhaa za gari hilo angani."

Prof Wright, kwa upande wake, anasema si rahisi gari hilo kujigeuza kuwa ndege kama inavyoonekana.

Changamoto za kiteknolojia ni kimoja tu cha vikwazo vingi vilivyopo katika kutengeneza magari yanayopaa angani. Uhalalishaji na utoaji vibali wa magari hayo kutumika rasmi huenda ukawa utaratibu mrefu na mzito sana, kama ilivyo kwa ndege za kawaida.

Itamlazimu dereva wa gari hilo kuwa na leseni ya urubani. Hata hivyo, Bw Dukhovny anasema katika njia za kuepuka vikwazo vingi, huenda idara husika zikaruhusu matumizi ya leseni za droni.

Huenda idara za serikali pia zikaweka masharti makali kuhusu maeneo ambako magari hayo yanaweza kuendeshwa angani.

*- Imetafsiriwa na Kamau Wanderi*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ SEKTA HIYO INA HISTORIA ILIYOANDIKWA YA UFISADI



Mwanamke atembea juu ya mabomba ya mafuta karibu na kituo cha kampuni ya mafuta ya Shell cha Utorogu, eneo la Warri, Nigeria. Serikali inasema dola za Amerika $3.3 bilioni (karibu Sh400 bilioni) zimepotea kutokana na wizi wa mafuta ambayo hayajasafishwa tangu mwaka uliopita, wakati ambao nchi zingine zinazotoa mafuta zinaendelea kutajirika kutokana na bidhaa hiyo.

# WIZI WA MAFUTA NIGERIA

*Katika jimbo la Delta, wezi walitengeneza bomba lao lenye urefu wa kilomita 4 kupitia mikondo iliyo chini ya ulinzi mkali hadi kufikia Bahari ya Atlantic. Hapo, meli na vyombo vya usafirishaji vilipakia hadharani mafuta yaliyoibwa kutoka kwenye chombo cha urefu wa futi 24 kinachoonekana maili kadhaa kikielea majini*

• LAGOS

Mtandao wa mifereji haramu ya mafuta inayochimbuliwa katika eneo la Niger Delta la Nigeria umefichua upeo wa wizi wa mafuta katika taifa hilo, na kuwaacha na mshangao hata walio wabishi wakuu kuhusu sekta ya mafuta inayogubikwa na utata lakini faida kuu Nigeria.

Katika jimbo la Delta, wezi walitengeneza bomba lao binafsi lenye urefu wa kilomita 4 (maili 2.5) kupitia mikondo iliyo chini ya ulinzi mkali hadi kufikia Bahari ya Atlantic. Hapo, meli na vyombo vya majini vilipakia hadharani mafuta yaliyoibwa kutoka kwenye chombo cha futi 24 kinachoonekana kutoka maili kadhaa kikielea kwenye maji makuu.

"Ilikuwa kazi ya kitaalamu," akasema mkuu wa Kampuni ya Kitaifa Petroli Nigeria (NNPC), Mele Kyari, akipitia kwenye vinamasi huku akifuatilia mkondo huo ulioundwa kwa weledi wa kupigiwa mfano wakati wa ziara iliyopeperushwa moja kwa moja katika televisheni.

Mafuta ambayo hayajasafishwa ndiyo bidhaa inayoongoza kwa mapato ya kigeni Nigeria lakini uzalishaji, na mapato, yamekuwa yakishuka kwa miaka mingi kwa sababu ya wezi, serikali inasema. Uzalishaji wa mafuta ulishuka kutoka mapipa 2.5 milioni kwa siku mnamo 2011 hadi zaidi ya milioni moja tu mnamo Julai 2022, kulingana na NNPC.

Serikali inasema Mamlaka zaidi ya dola $3.3 bilioni za amerika (karibu Sh400 bilioni) zimepotea kupitia wizi wa mafuta ambayo hayajasafishwa tangu mwaka jana na wakati huu ambapo mataifa mengine yanayozalisha mafuta yanaendelea kutajirika kutokana na raslimali hiyo, Nigeria haiwezi hata kutimiza kiwango chake cha uzalishaji. Na sio kwamba taifa hilo limejitosheleza kiasi cha kumudu kupoteza hela hizo kwa wezi, lina umaskini mkubwa na madeni chungu nzima.

Wengi wanasema kuwa uvumbuzi wa hivi majuzi wa mabomba haramu unathibitisha tuhuma ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu kuhusu uozo uliokita mizizi katika sekta hiyo yenye kiwango kidogo cha uwazi.

Sekta ya mafuta Nigeria ina historia Dhahiri ya ufisadi, kuanzia mpango wa ruzuku isiyoisha ya mafuta ambayo hakuna anayefahamu kiasi kinachonunuliwa kutoka nchi za kigeni, hadi ugavi wa visima vya mafuta unaogubikwa na usiri mkubwa.

Hali kwamba kashfa hiyo iligunduliwa na shirika la kibinafsi la ulinzi na sio serikali imechochea hasira zaidi.

Lakini Ekpemupolo, maarufu kama Tompolo, si mwanakandarasi wa kawaida wa kibinafsi wa ulinzi. Chifu huyo mwenye umri wa miaka 51 kutoka ufalme wa Gbaramatu, Jimbo la

...Endelea Uk 26

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya afrika

# Mabomba haramu ya mafuta yasumbua Nigeria

Kutoka Uk 25

Delta lenye utajiri wa mafuta awali alihusika na ulipuaji wa mabomba hayo ya mafuta ambayo sasa analinda baada ya kandarasi iliyokumbwa na utata ya naira bilioni 48 za Nigeria (karibu Sh13 bilioni) kutoka kwa serikali mwishoni mwa Agosti.

Inaaminika ndiye mpiganiaji wa zamani wa mafuta tajiri zaidi nchini Nigeria na wakati mmoja alikuwa mtu aliyesakwa zaidi nchini humo. Wakati mmoja aliuzia taifa hilo shehena ya silaha za kivita.

Pia anafahamu vyema mazingira ya Niger Delta, visima vya mafuta na mabomba rasmi ya mafuta, kwa hivyo wengi wanaamini madai yake kuhusu wanaohusika na wizi huo.

"Walinda usalama wengi wanahusika kwa sababu hakuna jinsi unaweza kupakia chombo bila kuwahonga walinda usalama wa eneo hilo," akaambia mashirika ya televisheni.

Alisema kiasi kikubwa cha mafuta kiliibiwa katika maeneo kuliko na vituo vya ukaguzi vya wanajeshi nchi kavu na wa majini.

Jeshi halijajibu madai hayo, lakini huenda halitamkosoa hadharani mwanamme ambaaye wameshirikiana naye kukomesha wizi wa mafuta.

Lucky Irabor, mkuu wa ulinzi Nigeria, aliyekuwa sehemu ya kikosi kilichozuru mikondo yenye mafuta ya wizi akisindikizwa na watu wa Tompolo, alisema ziara hiyo ilikuwa ya "kufungua macho" na akaahidi uchunguzi.

Lakini si mara ya kwanza vikosi vya usalama Nigeria, hasa maafisa wakuu wa jeshi la nchi kavu na jeshi la majini, wanalaumiwa kuhusu wizi wa mafuta.

Mnamo Januari, Nyesom Wike, gavana wa jimbo la River, alisema mkuu wa polisi alihusika na wizi wa mafuta katika eneo la Emuoha na alitaka atimuliwe.

Mnamo 2019, Bw Wike pia alimshutumu kamanda wa cheo cha juu kwa kujihusisha na biashara kubwa ya wizi wa mafuta katika jimbo hilo, madai yaliyokanwa. Hali kuwa ufisadi wa kiwango hiki ulifanyika chini ya uongozi wa Rais Muhammadu Buhari, ambaye pia ni Waziri wa Petroli Nigeria, imetilia shaka juhudi zake za kupigana na ufisadi, alisema Saludeen Hashim wa Hazina ya CLEEN Foundation, shirika lisilo la kiserikali la kupigana na ufisadi. Bw Buhari alichaguliwa kwa ahadi ya kupambana na ufisadi mnamo 2015, lakini wengi wanahisi kuwa utawala wake umeshindwa kuzima uovu huo.



Wanaume wawili wakiwa katika kiwanda kidogo cha kusafisha mafuta kinachotumiwa na wezi wa mafuta katika jimbo la Bayelsa, eneo la Niger Delta.

"Huenda kiwango cha wizi wa mafuta unaoendelea hakitajulikana hadi serikali hii itakapotoka ofisini Mei," mchanganuzi akaambia shirika la habari la BBC.

Tangu ilipate uhuru mnamo 1960, Nigeria imekuwa ikiongozwa mara kwa mara na wanajeshi wanaonyakua mamkala kupitua mapinduzi ya serikali, na kuacha nyuma uozo wa ufisadi unaofadhiliwa kupitia sekta kubwa ya mafuta na gesi katika Niger Delta.

Kutumwa katika eneo hilo kulinda vituo vya mafuta, kunachukuliwa kuwa biashara kubwa na maafisa wote, wakuu kwa wadogo ambao wengi hulipa hongo ili kupata nafasi hiyo, anasema Hashim.

"Wkifika huko tu huanza mbio za kuelekea chini kuzoa utajiri haramu," akaongeza. Kisa cha hivi majuzi cha kuteketezwa kwa meli iliyokamatwa kwa madai ya kubeba lita 650,000 za mafuta ambayo hayajasafishwa yaliyokuwa yameibwa katika jimbo la Delta pia kimeibua maswali. Wengi walishangaa ni kwa nini maafisa wa usalama walikuwa na haraka ya kuharibu ushahidi – sehemu ya ufanisi wa hivi punde wa Tompolo – lakini waziri wa ulinzi Nigeria alisema maadamu meli iliyokamatwa ilihusika imebeba mafuta yaliyoibwa, hakuna uchunguzi uliohitajika.

Ari ya Tompolo ya kukomesha wizi wa mafuta ambayo hayajasafishwa imeshangaza wengi. Analipwa kwa kazi hiyo, na ameelezea mapenzi yake kwa Nigeria na mazingira Niger Delta, lakini ni Tompolo yule yule, wanasema wengi, aliyelipua mabomba ya mafuta zamani.

Kama alivyosema mtaalamu mmoja, mabomba haramu ya mafuta yanayofichuliwa na Tompolo kufikia sasa yako katika jimbo la Delta, ambako anajivunia mamlaka makuu.

Haiwezekani kuna mtu aliyeendesha kwa Amani shughuli kama hizo katika eneo lake kwa miaka mingi bila yeye kujua, wanasema.

Awali, kumekuwa na mapigano makali katika vikosi vya usalama na wanamgambo wanaoendesha shughuli zao eneo hilo lakini mambo yametulia kwa miaka kadhaa, na wengi wanasema kuwa ni mkataba baina ya pande zote mbili kutoingilia "biashara" za mwingine.

Wanaopoteza, yamkini, ni raia wanaozingatia sheria wa Nigeria, na labda kampuni za mafuta. Si eti kwamba watapata huruma nyingi katika taifa hilo. — ***BBC***

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*



Kituo cha kampuni ya Shell cha mafuta na gesi katika Kisiwa cha Bonny, kusini mwa eneo la Niger Delta, Nigeria.

Nation Media Group "ePaper Copy"

# kurunzi ya dunia

■ JE, NETANYAHU ATAREJEA UONGOZINI BAADA YA UCHAGUZI ISRAELI?

# 'BIBI' APAMBANA KURUDI



Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Israeli, Benjamin Netanyahu, akihudhuria hafla kabla ya kumpa chanjo ya kwanza ya Covid-19 raia wa milioni 5, jijini Tel Aviv, Israeli, mnamo Machi 8, 2021. PICHA I MAKTABA

*Kura za maoni zinaonyesha atahitaji kuungwa mkono na mrengo wenye msimamo mkali wa kulia ili kubuni serikali – jambo ambalo, mdadisi mmoja alionya, litakuwa "mkasa" kwa demokrasia nchini Israeli*

• JERUSALEM

Huku Israeli ikitarajiwa kufanya uchaguzi mkuu wa tano chini ya miaka minne, swali moja linaibuka: Je, huenda aliyekuwa Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu akafanikiwa kurudi uongozini?

Kura za maoni zinaonyesha atahitaji kuungwa mkono na mirengo ya kulia ili kubuni serikali – jambo ambalo, kulingana na mdadisi mmoja, litakuwa "mkasa" kwa demokrasia nchini Israeli.

Netanyahu alikuwa waziri mkuu kwa jumla ya miaka 15, hiyo ikiwa rekodi ya kipekee katika miaka 74 ya historia ya taifa hilo. Kiongozi huyo aling'olewa mamlakani Juni 2021 na muungano wa vyama kadhaa vya upinzani vilivyokuwa vikimpinga.

Netanyahu anafahamika na wengi kama 'Bibi' na alikuwa mshirika wa karibu wa aliyekuwa rais wa Amerika, Donald Trump. Wakati wa uongozi wake, siasa za Israeli zilielekea katika mrengo wa kulia huku mazungumzo yote ya kutatua mzozo kati ya Israel na Wapalestina yakikwama.

Licha ya kukumbwa na mashtaka ya ufisadi, anayokana, kiongozi huyo ameapa kurudi katika ulingo wa siasa, bila kujali iwapo atafaulu katika juhudi zake au la.

Netanyahu, 73, ambaye ni kiongozi wa chama cha Likud, analenga kutumia migawanyiko inayokumba muungano wa kisiasa ulio mamlakani kurudi uongozini.

Muungano huo unajumuisha viongozi wenye miegemeo ya kidini, vyama vyenye mirengo ya kati na kushoto na chama huru cha Kiarabu - hilo likishuhudiwa kwa mara ya kwanza nchini humo.

Netanyahu alivuruga uthabiti wa muungano huo kwa kuagiza washirika wake katika bunge kupiga kura kupinga kupitishwa kwa mswada uliohakikisha Wayahudi wanaoishi eneo la West Bank wangeishi chini ya sheria za Israeli. Hiyo ni licha ya washirika wengi katika muungano huo kuunga mkono mswada huo.

Netanyahu aliamini muungano huo un-

Endelea Uk 28

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

# Macho kwa Netanyahu katika uchaguzi Israeli




**Wafuasi wa kiongozi wa chama cha Likud, Benjamin Netanyahu, ambaye pia alikuwa Waziri Mkuu wa Israeli, wakihudhuria mkutano wa kampeni katika mji wa Tirat Carmel, kaskazini mwa Israeli, mnamo Oktoba 25, kabla ya Uchaguzi Mkuu baadaye Novemba.**

Kutoka Uk 27

gegawanyika kutokana na mswada huo tata. Naftali Bennet alijiondoa kama Waziri Mkuu mnamo Juni, akisema hangeendelea kuongoza serikali. Waziri wa Mashauri ya Kigeni, Yair Lapid, alichukua usukani kama Kaimu Waziri Mkuu, huku uchaguzi mkuu ukipangiwa kufanywa nchini humo Novemba 1.

Ingawa kuvunjika kwa muungano huo kulikuwa ishara ya ushindi kwa Netanyahu, kura za maoni zinaonyesha huenda ikawa kibarua kwake na washirika wake kupata viti 61 katika Bunge (Knesset).

Kimsingi, inaonekana huenda Netanyahu hatafanikiwa kupata ushindi bila kuungwa mkono na mrengo wenye msimamo mkali wa kulia unaoitwa Muungano wa Kizayuni.

Muungano huo unamjumuisha Itamar Ben-Gvir, aliye na historia ya kutumia kauli za kuwakashifu Waarabu na ambaye ameeleza kumuunga mkono Baruch Goldstein, aliyehusika katika mauaji ya mamia ya Wapalestina katika mji wa Hebron, eneo la West Bank.

"Uchaguzi huu pengine ndio wenye utata zaidi kwani Netanyahu ameungana na chama cha kibaguzi, hali ambayo huenda ikawa pigo kubwa kwa demokrasia nchini humu," akasema Gayil Talshir, mwanasayansi wa siasa katika Chuo Kikuu cha Hebrew, Jerusalem.

"Huenda hii ikawa serikali yenye msimamo mkali zaidi wa kulia ambayo imewahi kushuhudiwa nchini humu," akaambia shirika la habari la AFP.

Lapid, 58, anayeongoza chama cha Yesh Atid, ameungwa mkono kwa wingi katika wakati mfupi ambao amehudumu kama Waziri Mkuu wa Mpito. Alimualika Rais Joe Biden wa Amerika, akakutana na Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa jijini Paris, Chansela Olaf Scholz wa Ujerumani jijini Berlin, na akafikia mkataba kuhusu eneo tata la mpakani na Lebanon.

Lapid pia alifanikisha operesheni kali ya kijeshi dhidi ya wapiganaji wa Kiislamu katika Ukanda wa Gaza. Operesheni hiyo, ambayo ilichukua siku tatu, ilifaulu kwa kiwango kikubwa. "Lapid aliamua kutazama uchaguzi huu kutoka mbali sana," akaeleza mwandishi Nahum Barnea katika gazeti maarufu la 'Yediot Ahronot.'

"Aliacha kila mmoja akafanya makosa na kujipaka tope, kisha akayalainisha kiungwana. Mwelekeo huo ndio uliosaidia chama cha Yesh Atid kuongeza umaarufu wake katika kura za maoni. Lakini haukuusaidia mrengo unaompinga Netanyahu."

Wiki iliyopita, kura za maoni zilionyesha kuwa Yesh Atid kingeshinda viti 24, hiyo ikiwa idadi kubwa kwa chama kimoja. Hata hivyo, nia ya mrengo huo kunyakua viti 61 inaonekana kukumbwa na changamoto kadhaa, kwani utahitaji kufanya makubaliano mengine ya kisiasa na vyama pinzani.

Chini ya utaratibu wa uwakilishi nchini Israeli, ni lazima chama ama muungano unaoshinda ushinde kwa angalao asilimia 3.25 ya kura au viti vinne katika bunge.

Baadhi ya tafiti zimeonyesha vyama vitatu ya Kiarabu havina umaarufu mkubwa, hali ambayo huenda ikavifanya kurushwa nje ya bunge kwa kutokuwa na uwakilishi wowote. Vyama hivyo pia havijajiunga na mrengo wowote wa kisiasa. Huenda mwelekeo huo ukaupa ushindi mrengo wa Netanyahu.

Jumapili iliyopita, Netanyahu alikuwa akiwarai wafuasi wa Likud katika mji wa kaskazini wa Migdal Haemek, kumuunga mkono. Aliwaambia wafuasi wake wajitokeze kwa wingi siku ya uchaguzi. "Nawasihi muwaambie marafiki zenu, majirani zenu na jamaa zenu wasiachwe nyumbani."

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

MAISHA YA KUKALIWA

# ‘SIMBA’ WATAMBA WEST BANK

*Ghasia kutokana na mzozo kati ya Israeli na Palestina zimeongezeka katika miezi ya hivi majuzi, hasa katika maeneo ya Nablus na Jenin, huku Isreali ikifanya mashambulio ya angani karibu kila siku katika eneo la West Bank, baada ya ongezeko la mashambulio dhidi ya Israeli*



Wanamgambo wa Palestina wakihudhuria mazishi ya watu waliouawa kwenye shambulio la usiku lililotekelezwa na Israeli katika mji wa Nablus, eneo la West Bank, mnamo Oktoba 25. Waziri Mkuu wa Israeli, Yair Lapid, alisema kuwa Wadih Al Houh, kiongozi wa kundi jipya la wanamgambo linalojulikana kama “The Lions’ Den”, ni miongoni mwa waliouawa.

• NABLUS, PALESTINA

Droni za Israeli zinazunguka angani katika mji wa Nablus. Wanajeshi wa Israeli wanafunga barabara za kuingia jiji la West Bank na taharuki kutanda huku kukiwa na mazungumzo kuhusu kuzuka kwa “intifada” mpya.

Vijana Wapalestina wanaendesha kwa kasi pikipiki wakipita kando ya wauzaji bidhaa tofauti yakiwemo mafuta ya mzeituni hadi sindiria, huku wamevaa mavazi ya rangi za mashujaa wao wapya - “Areen al-Ossoud” au “The Lions’ Den” kwa Kiingeza na kiongozi wao, marehemu Ibrahimu al-Nabulsi.

Kijana Nabulsi, ambaye kwa jina la utani aliitwa “The Lion of Nablus” (Simba wa Nablus) alikuwa maarufu kwa kushirikisha vijana kabla ya kifo chake Agosti na sasa amekuwa shujaa kwa Wapalestina katika mitandao ya kijamii.

Baada ya kifo chake, wapiganaji wachanga wanaoegemea makundi kama Fatah, Islamic Jihad na Hamas walibuni muungano uliojulikana kama “The Lions’ Den” (Pango la Simba).

Umaarufu wake ulienea kama moto nyikani katika eneo zima la Himaya ya Palestina, kupitia mtandao wa mawasiliano wa Telegram.

Kwa nini mpiganaji mmoja mchanga kwa jina Abu Oday alijiunga na Areen Al-Ossoud? “Kwa sababu kundi hilo limeamua kutumia silaha kuzuia kutekwa kwa eneo hilo,” akaambia AFP. “Sisi ni kundi dogo na tunakabiliwa na hatari ya kuuawa, kwa hivyo kitakachotokea baadaye kitategemea atakayeungana nasi,” akaongeza.

Wiki hii, Simba walitumia Telegram kutoa wito kwa wafuasi wake karibu 180,000 kushiriki maandamano ya kila usiku katika eneo zima la West Bank.

Ghasia kutokana na mzozo kati ya Israeli na Palestina zimeongezeka miezi ya hivi majuzi, hasa katika maeneo ya Nablus na Jenin, huku Isreali ikifanya mashambulio ya angani karibu kila siku katika eneo la West Bank.

Wapiganaji zaidi ya 115 wa Palestina na raia waliuawa mwaka huu, idadi kubwa zaidi kuwahi kutokea eneo la West Bank katika miaka saba, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN).

Idadi hiyo ya waliouawa ni ya juu zaidi tangu mwisho wa “intifada” ya pili au mapinduzi ya mapema miaka ya 2000. Hiyo ilifuatia intifada ya kati ya 1987 na 1993 iliyochangia kufikiwa kwa mwafaka wa Oslo.

“Huu unaweza kuwa mwanzo wa intifada mpya,” akasema Khader Adnan, mwenye umri wa miaka 44. Adnan ni kiongozi maarufu wa kundi la Islamic Jihad katika eneo la Kaskazini mwa West Bank, ambaye amefungwa jela mara kadhaa na serikali ya Israeli.

“Areen Al-Ossoud wanaungana kuendesha upinzani. Vijana hawa hawategemei udhamini wa kundi lolote. Wanaonyesha kuwa kuendesha upinzani ni muhimu kuliko vuguvugu lolote,” akaambia AFP.

Abu Mustafa, alyepigana katika intifada ya kwanza, alisema Wapalestina wachanga “wanaishi chini ya uvamizi wa Israeli bila matumaini na kazi”. “Kwa intifada ya tatu kutokea, ni lazima pawe na makubaliano miongoni mwa makundi mbalimbali,” akasema.

“Lakini hivyo sivyo ilivyo: Hamas inataka kutambuliwa kimataifa. Fatah inashikilia mamlaka na kundi la Islamic Jihad ni Islamic Jihad, lilikuwa tayari jana, liko tayari leo na litakuwa tayari kesho”.

Makabiliano yanafanyika hasa kaskazini mwa West Bank. Lakini Adnan anaamini yanaweza kusambaa katika maeneo mengine, ikiwa kwa mfano, wanajeshi wa Israeli watamuua Fathi Hazem.

Mwanawe Hazem, Raad aliwaua Waisraeli watatu kwenye ufyatulianaji risasi katika barabara yenye shughuli nyingi ya Disengoff, jijini Tel Aviv, Aprili 7. Baadaye aliuawa kwa kupigwa risasi. Hazem ni “zaidi ya shujaa - ni kiongozi halisi,” akasema Adan. Kama angeuawa, “basi intifada ingekuwa imekamilika.”

Hazem ambaye ameorodheshwa miongoni mwa “Watu Wanaosakwa” zaidi na Israeli, alipoteza mwana wa pili wa kiume wakati wa uvamizi eneo la Jenin.

Waziri mkuu wa Palestina, Mohammad Shtayyeh, ambaye serikali yake imelaumiwa huku mazungumzo yakiendelea kuhusu utawala wa Palestina baada ya Abbas, juzi alifanya ziara ya nadra katika kambi ya Jenin. Akiwa huko, alionekana akiandamana na Fathi Hazem na wapiganaji waliokuwa na silaha hatari kuliko polisi wa Palestina.

Alisema mapigano yataendelea kutoka “kizazi hadi kizazi” na kuilaumu Israeli kwa kuendelea kukalia eneo hilo tangu 1967.

Waisraeli zaidi ya 475,000 sasa wanaishi katika makao ya West Bank ambayo ni haramu kulingana na sheria za kimataifa. Tor Wennesland, Mshirikishi wa Umoja wa Mataifa kuhusu Amani Mashariki ya Kati, pia amezuru Nablus na Jenin, katika juhudu za kupunguza uhasama katika West Bank.

Katika miaka ya hivi majuzi eneo hilo limegubikwa na vita katika Ukanda wa Gaza, eneo la Palestina linalokaliwa na kundi la Kiislamu la Hamas.

Jeshi la Israeli liliambia AFP kuwa limefanya mashambulio zaidi ya 2,000 katika eneo hilo tangu Machi “kuzuia ugaidi kabla ufike Israeli”. — ***AFP***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## TANZIA

■ AMEACHA KUMBUKUMBU KATIKA NYANJA TOFAUTI ZA UTUMISHI WA UMMA

# NYOTA WA 'LATE DATE' APUMZIKA

*Sauti nzito ya kuliwaza ya George Opiyo ilikuwa ya kipekee na angecheza nyimbo tamu ambazo alisema zilikuwa 'moto kama kachumbari ya viazi'*

● Na BILL ODIDI

Mtangazaji, mwanahabari, mtayarishaji wa muziki, wakili na balozi. Ndiyo maelezo halisi ya maisha ya George Opiyo, aliyekufa Oktoba 19, na kuacha kumbukumbu katika nyanja tofauti za utumishi wa umma.

Opiyo alikuwa maarufu miaka ya mapema ya 1970, alipoongoza shoo maarufu za redio katika Idhaa ya Kiingereza ya Sauti ya Kenya (VOK), ambayo kwa wakati huu inaitwa Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC), akisomea sheria katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

"George alikuwa na mtindo wa kipekee, kila wakati aliivaa mavazi rangi nyeusi kutoka kichwani hadi mguuni na alikuwa akibeba mkoba mweusi," anakumbuka Abdul Haq, rafiki na waliyefanya kazi pamoja Idhaa ya Kiingereza.

"Hakuwa akiropokwa akiwa hewani, lakini kila wakati alikuwa na ujumbe na alifanya utafiti mwingi kuhusu kila muziki aliocheza," anasema Haq.

"Alimpenda Barry White, na hata pengine alitamani kuwa na sauti nzito kama ya mwanamuziki huyo maarufu wa Amerika."

Opiyo alipeperusha vipindi vya Breakfast Club, Late Date na Yours for the Asking. "Shoo yake ya Yours for The Asking ilikuwa tofauti kwa sababu alizungumza moja kwa moja na wasikilizaji, kana kwamba alikuwa akiwasiliana ana kwa ana nao," anakumbuka Haq. "Tulikuwa marafiki walioshindana kwa umaarufu."

John Sibi Okumu alikuwa akisoma habari katika Idhaa ya Kiingereza miaka ya 1970 na anamtaja George Opiyo kuwa "Bwana Mtulivu" wa enzi hizo: "Sauti yake katika Late Date ilikuwa ya kipekee na angecheza vibao vya kuvutia ambavyo anakumbukwa akisema vilikuwa "moto kama kachumbari ya viazi."

Kazungu Katana, aliyejiunga na VOK mnamo 1973, anasema alinufaika kutokana na ulezi wa Opiyo. "Alikuwa mtu wa watu lakini pia aliyechagua marafiki na nilikuwa na bahati kuungana naye kama mwenzangu na pia rafiki," anasema Katana.

"Alitumia ufahamu wake wa sheria na lugha kusaidia wafanyakazi wenzake wengi kujibu barua zilizolenga kuwachukulia hatua za kinidhamu, hasa alipohisi hapakuwa na sababu nzuri za hatua kama hiyo kutoka kwa wakubwa," anasema Lenny Mwashegwa, mtangazaji mwingine maarufu wa VOK.

Katika kumbukumbu yake binafsi inayoitwa 'The Long Journey for Survival', George Opiyo Obong'o alizaliwa mnamo 1951 katika kijiji cha Kamunda, Awasi, Kisumu, akiwa wa tatu katika familia ya watoto wanane.

Baba yake alikufa akiwa na umri wa miaka saba na mama yake, aliyekuwa akiugua, akampeleka yeye na kaka zake wawili katika shule ya msingi ya Awasi, ingawa alikuwa akiacha masomo kufanya vibarua kusaidia familia.

Wakati mmoja aliacha shule na kwenda kuishi na dada yake katika mashamba ya mikonge ya Koru, ambako alikuwa akilipwa shilingi tisa kwa mwezi. Mama yake alikataa na akamrudisha shule. Baadaye Opiyo alijiunga na Shule ya Msingi ya Gendia huku akifanya kazi katika nyumba ya raia wa Uganda katika Kendu Mission Publishing House.

Mwaka wa 1966, alijiunga na shule ya The Prince of Wales (ambayo sasa ni Nairobi School), ambako alikuwa akipata pesa kwa kuoshea walimu magari yao wikendi. Mkuu wa bweni lake la Rhodes House, Keith Harrington, alikuwa wa kwanza kumiliki 'kituo cha kuoshea magari'.

Mapema miaka ya 1970, wakati wa kurekodi vipindi vya shule katika VOK, kijana George Opiyo alimvutia Peter Clare, aliyekuwa Mkuu wa Idhaa ya Kiingereza, na akamualika katika kituo hicho kuongoza vipindi vya burudani.


"Chaguo langu la muziki katika kipindi cha Late Date lilipokewa vyema na kunifanya maarufu miongoni mwa wakubwa wangu," aliandika. "Muda si mrefu, nilikuwa mtangazaji katika VOK na hii ikawa kazi niliyokuwa nikilipwa vyema wakati huo."

Pia aliandika makala katika gazeti la Daily Nation yaliyoitwa Teen Time, "ambayo yalinipa pesa nyingi… bajeti ya mama yangu maskini iliimarika sana".

Shabiki wake kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi alimtambulisha kwa bendi kutoka Congo, Les Mangelepa, iliyokuwa ikitumbuiza katika Garden Square, Nairobi. Kiongozi wa bendi hiyo, Evany Kabila wa Kabanze, anakumbuka alimuona Opiyo kwa mara ya kwanza alipoenda Aquarius Club, Ngara, kumhoji Baba Gaston Ilunga wa Ilunga.

"Alikuwa meneja wetu tulipotengana na Baba Gaston na kuunda Mangelepa. Alitusaidia kutia saini mikataba ya kusambaza muziki wetu na Phares Oluoch Kanindo, EMI Records na Polygram," anakumbuka Kabanze.

Kufikia wakati huo, Opiyo alikuwa ameanzisha kampuni yake ya JoJo Productions na mwaka wa 1976, Mangelepa ilitoa rekodi kadhaa chini ya kampuni hiyo kama vile Ekubuku, Sakina, Aoko, Mangelepa Kamili na Naleli Papa. Aliitiwa kazi katika East African Records (Polygram), ambayo alikataa kwa sababu alikuwa amebakisha mwaka mmoja kabla ya kuhitimu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi.



George Opiyo

Alipopata digrii yake ya sheria, Opiyo aliajiriwa rasmi kuwa mtayarishaji wa vipindi katika VOK. Mwaka huo, mvumishaji wa sherehe, Sam Ngugi, alikuwa amerudi kutoka Japan akiwa na baadhi ya vifaa bora vya disko wakati huo na akamuajiri Opiyo kuwa DJ wa shoo zake kote nchini.

Alijiunga na Idhaa ya Afrika ya Radio Deutsche Welle jijini Cologne, Ujerumani, kwa kandarasi ya miaka minne.

Aliporudi 1987, Opiyo aliteuliwa na Wizara ya Habari kusimamia uhusiano wa umma katika Michezo ya Nne Barani Afrika iliyofanywa Nairobi na baadaye akatumwa kuwa Afisa wa Habari katika Ubalozi wa Kenya, Stockholm, Uswizi. Alirudi katika Wizara ya Habari baada ya muhula wake katika ubalozi na akapanda cheo kuwa Mkurugenzi wa Habari.

Baada ya kustaafu, alihudumu katika Tume ya Filamu ya Kenya na kazi yake ya mwisho ya umma ilikuwa Mshauri Mkuu katika Kenya Yearbook Editorial Board. Alihamia Awasi mwishoni mwa 2020 kufanya kazi ya uwakili.

"Alihusika katika kesi nyingi za urithi bila malipo kama njia ya kusaidia jamii," anasema mwanawe kitinda mimba, Joash.

Opiyo alifariki akiwa katika hospitali ya Mafunzo na Rufaa ya Jaramogi Oginga Odinga ,Kisumu, alikokuwa akitibiwa Nimonia. Katika kumbukumbu zake, alisema: "Namshukuru Mungu kuwa mvulana asiye baba, ambaye maisha yake ya kazi yalianza katika stoo ya mikonge Awasi, ametumia miaka yake mingi akipambana kufaulu na pia kuhakikisha familia yake inaishi maisha ya heshima."

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep





**SMS the word GAZETI to 20567,**
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE SMS text and FREE Delivery**

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM